LAMBETH CONFERENCE

Kanisa la Mungu kwa Dunia ya Mungu

# WITO WA LAMBETH

Kilichapishwa Mei 2023, kama sehemu ya awamu ya tatu ya safari ya Lambeth Conference

# UTANGULIZI

Lambeth Conference ilikutana mwaka 2022 ili kuchnguza mada 'Kanisa la Mungu kwa Dunia ya Mungu – Kutembea, Kusikiliza na Kushuhudia Pamoja.'

Wakati wa kongamano hilo, miito kumi ya Lambeth ilijadiliwa na maaskofu kuhusu mada za kanisa na masuala ya ulimwengu.

Mada ya miito ya Lambeth ni:

- Uanafunzi
- Mazingira na Maendeleo Endelevu
- Utambulisho wa Anglikana
- Kanisa Salama
- Sayansi na Imani
- Heshima ya Binadamu
- Umoja wa Kikristo
- Utume na Uinjilisti
- Uhusiano Baina ya Imani
- Maridhiano

Miito ya Lambeth imeandaliwa kufuatia muundo unaojumuisha:

- Tamko, likifupisha kile ambacho Kanisa la Kikristo limefundisha kwa ujumla kuhusu mada ya wito.
- Uthibitisho, ukifupisha kile maaskofu wanachotaka kusema kuhusu mambo ya wakati huu.
- Maombi maalum (Miito) kwa ushuhuda wa baadaye, kushirikishana kwa hatua au changamoto ambazo maaskofu wanataka kupeana wao kwa wao, kwa Wakristo wenzao na kwa ulimwengu.

Miito ya Lambeth iliwasilishwa kwa maaskofu katika mkutano wa Julai-Agosti 2022. Kila Wito wa Lambeth ulianzishwa na kikundi cha uandaaji kilichoundwa na maaskofu, makasisi na walei kutoka Ushirika wa Anglikana, wakiongozwa na Padri au askofu mwandamizi.

Toleo hili la Miito ya Lambeth, lililochapishwa mwaka wa 2023, linabebamabadiliko yaliyofanywa na vikundi vya uandaaji kufuatia maoni yaliyotolewa na maaskofu katika Lambeth Conference mwaka wa 2022.  Miito inatolewa katika utaratibu tofauti na ule uliokuwepo kwenye kongamano, ili kuiunganisha kwa karibu zaidi na majira ya mwaka wa kikristo na matukio makubwa ya kimataifa.

Miito hii sasa songeshwa katika Awamu ya 3 ya safari ya Lambeth Conference.

Lambeth Conference ni 'Chombo cha Ushirika' na kwa hivyo, Miito ya Lambeth hutolewa kama zawadi, kwa Ushirika wa Anglikana. Inakusudiwa kuchunguzwa na makanisa na jamii na songeshwa kwa namna ambayo inafaa zaidi kwa mazingira ya mahali husika.

Kwa taarifa, soma **kuhusu Miito ya Lambeth na Awamu ya 3 ya safari ya kongamano**, pamoja **Historia na Kusudi la Lambeth Conference** kwenye tovuti.

Lengo la kila wito ni kuimarisha uaminifu kwa Mungu, kuendeleza huduma ya Ushirika na kuwezesha ushiriki mkubwa katika wito wa makanisa na jumuiya duniani kote.

LAMBETH CONFERENCE
Kanisa la Mungu kwa Dunia ya Mungu

# YALIYOMO


WITO WA LAMBETH KUHUSU UANAFUNZI 4

WITO WA LAMBETH KUHUSU MAZINGIRA NA MAENDELEO ENDELEVU 7

WITO WA LAMBETH KUHUSU UTAMBULISHO WA ANGLIKANA 13

WITO WA LAMBETH KUHUSU KANISA SALAMA 17

WITO WA LAMBETH KUHUSU SAYANSI NA IMANI 20

WITO WA LAMBETH KUHUSU HESHIMA YA BINADAMU 23

WITO W LAMBETH KUHUSU UMOJA WA KIKRISTO 28

WITO WA LAMBETH KUHUSU UTUME NA UINJILISTI 31

WITO WA LAMBETH KUHUSU UHUSIANO BAINA YA IMANI 33

WITO WA LAMBETH KUHUSU MARIDHIANO 36

# WITO WA LAMBETH
# **UANAFUNZI**

## 1 Utangulizi

1.1 Mfuasi ni mwanafunzi katika akili, mwili na roho. Katika Wito unaofuata, maaskofu waliokusanyika katika Lambeth Conference wanawaomba Waanglikana wote kujifunza na kujifunza tena namna ya upendo, ukombozi na kujitolea mhanga kwa Yesu Kristo katika kila nyanja ya maisha yao na kumfuata katika hili. Maaskofu wanatoa Wito huu kwa sababu 1 Petro huwaita watu wote wa Mungu kwenye uanafunzi kama huo wenye nidhamu na wa maisha yote:

*Kwa hiyo, andaeni nia zenu kwa kazi; muwe na kiasi, mkitumainia kikamilifu ile neema mtakayopewa Yesu Kristo atakapodhihirishwa. Kama watoto watiifu, msifuate tamaa zenu mbaya ambazo mlikuwa nazo wakati mlipoishi kwa ujinga. Bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, nanyi kuweni watakatifu katika mwenendo wenu wote. Kwa maana imeandikwa: "Kuweni watakatifu, kwa kuwa mimi ni mtakatifu.'*(1 Petro 1.13-16)

1.2 Huu ni wito unaohitaji juhudi zetu kubwa kwa sababu ya mashinikizo yanayokuja kwetu kutoka kwa jamii na vita vya kiroho vinavyowakabili wote. Lakini waraka huu unaonyesha kwamba tunaweza na tunapaswa kutegemea msaada wa Mungu:

*Mtu akisema, na aseme kama mausia ya Mungu; mtu akihudumu, na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu; ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo. Utukufu na uweza una yeye hata milele na milele. Amina.'* (1 Petro 4.11)

Basi, wito huu ni kwa Waanglikana wote katika kila nyaja ya maisha yao kujifunza na kujifunza tena njia ya Yesu Kristo 'kwa nguvu ambayo Mungu hutoa', nguvu inayotolewa na Roho Mtakatifu, na kumfuata yeye katika hili.

## 2 Azimio

2.1 Yesu aliwafundisha wanafunzi wake "Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi". Ukubwa na kiwango cha Ushirika wa Anglikana leo unaonyesha kwamba Waanglikana ulimwenguni kote wamekuwa wakifanya hivi katika historia yao yote kwa shauku na kujitolea.

2.2 Hata hivyo, baadhi ya watu wamesema kwamba ingawa kujizatiti kwa Kikristo 'ni upana wa maili lakini kina chake ni inchi moja tu.' Kwa mfano, katika maeneo mengi kujitolea kwa Wakristo kumeonekana kuwa ni Wakristo wa jina. Ili kukabiliana na hili Msimu wa Uanafunzi wa Makusudi na Ufanyaji Wanafunzi (Maisha yanayomwiga Yesu) ulizinduliwa katika Baraza la Ushauri la Anglikana huko Lusaka mwaka 2016:

*Kwa kuzingatia Injili na umuhimu wa kitheolojia wa kufanya wanafunzi, [sisi] tunatambua hitaji la kila jimbo, dayosisi na parokia katika Ushirika wa Anglikana kuchukua mwelekeo dhahiri juu ya ufuasi wa makusudi na kuzalisha rasilimali za kuandaa na kuwezesha kanisa lote kuwa na ufanisi katika kufanya wanafunzi wapya wa Yesu Kristo.* (ACC-16, Azimio la 16.01)[i].

2.3 Azimio hili lilithibitishwa tena mwaka 2019 katika ACC-17 huko Hong Kong. Msimu utaendelea hadi ACC-19 mwaka wa 2026. Hadi sasa zaidi ya dayosisi 100 na majimbo mengi kati ya 42 ya Ushirika wa Anglikana yamekubali hapo awali. Uanafunzi wa Makusudi kama kipaumbele muhimu na/au yameandaa mashauriano na warsha juu ya somo hili. Matumizi ya vikundi vidogo ni muhimu sana. Ushirika wa Anglikana umeandaa rasilimali nyingi za kusaidia Msimu na maisha yanayoongozwa na Yesu (**www.anglicancommunion.org/mission/intentional-discipleship.aspx**).

2.4 Makanisa mengine mengi ulimwenguni pia yanaitikia hitaji la kuimarisha uanafunzi. Wito wa Arusha wa Uanafunzi wa mwaka 2018, kutoka katika Baraza la Makanisa Ulimwenguni, ambalo Waanglikana walichangia, lilionyesha hili kwa nguvu wakati lilipotangaza kwamba 'Tumeitwa kupitia ubatizo wetu katika uanafunzi ubadilishao: maisha yaliyounganishwa na Kristo katika ulimwengu ambao wengi wanakabiliwa na kukata tamaa, kukataliwa, upweke, na kutokuwa na thamani.' [ii] Papa Francis pia amewaita watu wote wa Mungu kuwa wanafunzi wamishenari na ameufanya wito huu kwa kipaumbele katika huduma yake. [iii]

2.5 Kwa kuwa Waanglikana tumeingia katika Msimu wetu wa Uanafunzi wa Kukusudia wengi wamegundua kuwa Alama Tano za Utume hutoa seti ya ishara za kuhamasisha na kuunganisha kwa ajili ya kujifunza na kufuata njia ya Kristo. Kwa hiyo miito inayofuata inakaribisha Waanglikana kutengenezwa na alama hizi ili tuweze kuishi na kuonyesha maisha yanayoongozwa na Yesu zaidi na zaidi.

## 3 Uthibitisho

Sisi maaskofu waliokusanyika katika Lambeth Conference, katika Msimu huu wa Uanafunzi wa Kukusudia, tunajizatiti kujifunza na kujifunza tena namna ya upendo, ukombozi na maisha ya kujitoa mhanga ya Yesu Kristo katika kila nyanja ya maisha yetu, kwa njia ya sala, Neno na sakramenti, kwa nguvu ambayo Mungu hutoa, ili kumfuata kwetu kuimarishwe na Roho Mtakatifu na kwamba watu wa majimbo yetu wahamasishwe kufanya vivyo hivyo.

## 4 Maombi Maalum (Miito)

4.1 Tunatoa wito kwa Waanglikana wote, katika Msimu huu wa Uanafunzi wa Kukusudia, wajifunze na wajifunze tena namna ya upendo, ukombozi na maisha ya kujitolea mhanga ya Yesu Kristo katika kila nyanja ya maisha yetu, katika maisha ya kila siku, kwa njia ya sala, Neno na sakramenti, na katika vikundi vidogovidogo, kwa nguvu ambayo Mungu hutoa, ili kumfuata kwetu kuimarishwe na Roho Mtakatifu na kuwafanya wengine kuwa wanafunzi. Kuendehela kujifunza katika maisha huhitajika katika suala hili, tukifahamu wito wetu. Tunatoa wito hasa kwa Waanglikana watengenezwe na Alama Tano za Utume, kama Kanuni ya Maisha ya Ushirika wa Anglikana, kuwa mazoea yao kupitia udhihirisho wa mara kwa mara, kwa tafakari na kulingana na muktadha unaofaa:

- Tangaza - kutangaza Habari Njema ya Ufalme wa Mungu
- Fundisha - kufundisha, kubatiza na kulea waumini wapya
- Shughulikia - kushughulikia mahitaji ya wanadamu kwa huduma ya upendo ikiwa ni pamoja na kupitia huduma za uponyaji
- Badilisha- kutafuta kuleta mabadiliko ya mifumo ya jamii isiyo haki, kupinga vurugu za kila aina na kutafuta amani na mapatano;
- Thamini - kujitahidi kuuhifadhi ukamilifu wa uumbaji na kutunza na kufanya upya maisha ya dunia

4.2 Tunatoa wito kwa viongozi wote, wa kawaida na waliosimikwa, ili kuwezesha ibada zetu na liturujia kwa makusudi kuwa mahali ambapo tunatengenezwa na kubadilishwa katika akili zetu, mwili na roho kuishi maisha yanayoongozwa na Yesu, yaliyozingatia hasa katika agano la ubatizo la huduma ya Ubatizo, ambapo watu wapya waliobatizwa wanahakikishiwa msaada wa kusanyiko katika maisha yao mapya katika Kristo.

4.3 Tunatoa wito kwa dayosisi kusaidia pia parokia kuanzisha na kupanua vikundi vidogo kwa ajili ya malezi ya uanafunzi na kutoa na kusaidia 'malango' mengine kuingia katika uanafunzi katika maisha ya kila siku, mtandaoni na ana kwa ana, kulingana na mazingira yao, ikiwa ni pamoja na mahali pa kazi, shule na jumuiya. Rasilimali kwa ajili ya maendeleo ya watoto wadogo pia zinahitajika.

4.4 Tunatoa wito kwa wote katika makanisa yetu kuendeleza uhusiano wa kina na vijana kwa kukusudia, katika shule, makusanyiko na jumuiya, na kujifunza kutoka kwa wale ambao ni waandamizi katika uanafunzi wao, na kutoka kwa wanawake, watu waliotengwa na maskini, ili kujifunza na kubadilika huku kuweze kufanyika katika kanisa zima na kwa kila mtu kugundua karama zake kutoka kwa Kristo, kuzitumia kwa faida wanapomfuata.

4.5 Tunatoa wito kwa seminari zetu, vyuo vya kitheolojia na programu za mafunzo kufikiria kuweka umuhimu kwenye uanafunzi na kufanya wanafunzi, kuandaa upya mitaala ya mafunzo na kujifunza, ili wachungaji wote, waliosimikwa na walei, wapewe maarifa ya kuwawezesha wale wanaowatumikia kujifunza mambo haya, zaidi kwa njia ya kuhubiri;

4.6 Tunatoa wito kwa Katibu Mkuu wa Ushirika wa Anglikana kuhamasisha na kusaidia maendeleo katika maeneo haya kwa msaada wa Tume ya Uinjilisti na Uanafunzi, pamoja na kupitia kuhamasisha Msimu wa Uanafunzi wa Kukusudia kote kwenye Ushirika, na kuripoti kwenye ACC ijayo na Lambeth Conference ijayo kuhusu namna vile majimbo yanahamasisha kikamilifu uanafunzi wa kukusudia.

**5 Utekelezaji**

Katika kupokea na kutekeleza Wito huu, majimbo na dayosisi zitahitaji kufanya kazi zaidi katika maeneo maalumu, kwa mfano ni aina gani ya uundaji wa vikundi vidogo wa aina gani unavofaa zaidi katika muktadha wao? kuna uwezekano gani wa kuanzisha kanisa? na ni umahiri gani ambao vyuo, seminari, na kazu zinapaswa kuwapa wahitimu wao?

## Melezo ya Mwisho

i. ACC-16, Azimio la 16.01

ii. R. Jukko na J. Keum, *Kuenenda kwa Roho,* Geneva: WCC 2019

iii. *Evangelii Gaudium*, 2017

# WITO WA LAMBETH
# MAZINGIRA NA MAENDELEO ENDELEVU

## A. MAZINGIRA

**1 Utangulizi**

1.1 Tumejaliwa ulimwengu uliojaa uzuri, utele wa kushangaza na uhusiano wa kipekee. Ni ulimwengu ambao Mungu alitangaza kuwa ni mwema na anaupenda.

1.2 Ulimwengu huo sasa upo katika mgogoro. Mabadiliko ya hali ya hewa, kupotea kwa viumbe hai na uchafuzi wa mazingira hutishia watu na sayari. Pamoja na changamoto hizi za kimazingira, na mara nyingi zikichochewa nazo, kuna umasikini, ukosefu wa usawa, ukosefu wa haki na mzozo ambayo inaharibu maisha ya mamilioni ya watu.

1.3 Hata hivyo, hii bado ni dunia ya Mungu na Mungu anatuita tuitikie kama watu wa Pasaka: wabeba- matumaini.

1.4 Lambeth Conference ilijifunza kitabu cha 1 Petro. Katika andiko hili, tumeitwa “kuwa na upendo wa kweli” (1 Petro 1:22), unaoonyesha ukarimu, uwakili na huduma ya pamoja (diakonia) (1 Petro 4: 9-10). Haya ni mambo muhimu katika huduma ya kujaliana na maskani yetu ya pamoja, dunia.

1.5 Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu (dunia) hata akamtuma Mwana wake wa pekee ulimwenguni (Yohana 3:16). Duniani, Yesu alipata amani na utulivu katika ulimwengu wa asili pamoja na hamasa ya mafundisho yake. Yesu alikufa msalabani kuleta upatanisho kwa viumbe vyote. “Kwa kuwa katika yeye ilipendeza utimilifu wote ukae; na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake”. (Wakolosai 1:19-20)

1.6 Wakati changamoto za mazingira ni kubwa, hadithi ya Kikristo ni ya ukombozi, ufufuo, kubadilishwa na matumaini. Yesu anawaita wanafunzi wake kufuata Njia ya upatanisho na viumbe vyote na, kupitia Roho Mtakatifu, tunawezeshwa kufanya hivyo.

**2 Azimio**

2.1 Waanglikana wanashikilia Maandiko na mafundisho ya Kanisa, yaliyoonyeshwa katika Alama Tano za Utume. Haya hutoa maono dhahiri na mfumo kamili wa uanafunzi wa kukusudia na kwa kuwa Kanisa la Mungu kwa Dunia ya Mungu. Hutuita kutangaza Habari Njema ya ufalme, kulea wanafunzi, na kuelezea wasiwasi wetu kwa watu na sayari, kwa ajili ya haki, amani na utunzaji wa watu walio katika mazingira magumu na pia jukumu letu la kulinda uumbaji (Mwanzo 2:15) na kudumisha na kufanya upya maisha ya dunia (Alama ya Tano ya Utume).

2.2 Kwa hiyo Waanglikana hawazingatii tu ustawi wa binadamu na uumbaji, lakini pia wanaona haya kama mahitaji ya kiutume na jinsi tunavyoshiriki katika ‘uumbaji mpya wa mbingu na dunia pamoja na haki’ (2 Petro 3:13).

2.3 Uadilifu wa uumbaji uko chini ya tishio na uko katika hatari ya kuanguka. Haja ya kufanya Alama ya Tano ya Utume kuwa msingi wa maisha yetu kama Waanglikana ni muhimu zaidi. Theolojia ya utawala imetumiwa kuhalalisha tabia za unyonyaji na ukandamizaji, ambazo zimechangia migogoro ya sasa ya mazingira. Tunahitaji kutubiu uharibifu wa dhambi uliofanywa kupitia theolojia hizi na tujizatiti kubadilika, na kuwaongoza wengine kwa toba watubu.

2.4 Ushirika wa Anglikana unajenga juu ya urithi wa Lambeth Conference wa mwaka wa 2008, ambao ulionyesha kujizatiti sana katika Malengo ya Maendeleo ya Milenia ya Umoja wa Mataifa na kuzaa Umoja wa Anglikana. Pia unajenga kwenye ACC 17, ambayo ilithibitisha ahadi hii kwa kuzingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa [**https://sdgs.un.org/goals**].

2.5 Majimbo katika Ushirika wote yanaendelea kushughulikia changamoto za kijamii na mazingira za mahali husika, za kitaifa na kimataifa. Katika changamoto kuna fursa: kwa Kanisa kusikiliza sauti ya Mungu, kufikiria jinsi ulimwengu unaweza kuwa tofauti, na kusaidia kujenga Ufalme wa Mungu.

2.6 Lakini migogoro mitatu ya kimazingira ambayo ni mabadiliko ya hali ya hewa, kupotea kwa viumbe hai na uchafuzi wa mazingira ni tishio. Ikwa maisha ya mamilioni ya watu na aina za mimea na wanyama duniani kote. Jopo la Muunganiko wa Serikali la Mabadiliko ya Hali ya Hewa (IPCC) limeonya kuwa ni “ishara nyekundu kwa ubinadamu”; “Ni sasa au isitokee kabisa, ikiwa tunataka kupunguza ongezeko la joto kufukia 1.5 ° C”. [i] Hatua kubwa inahitajika katika miaka mitatu ijayo ili kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa ili kufikia lengo la kutozalisha tena hewa hiyo.

2.7 Kama mwili mmoja ulioenea duniani kote wenye utambulisho wa pamoja unaovuka mipaka ya kitaifa, Ushirika wa Anglikana una mtazamo tofauti. Makanisa wanachama wa Ushirika wa Anglikana wanahusika katika kila sehemu ya dharura ya mazingira. Sisi ni watu ambao tunakabiliwa na uharibifu katika jamii zilizokumbwa na maafa. Sisi sote ni wachafuzi wa mazingira, hasa katika nchi tajiri. Sisi ni watu tunaoishi katika umaskini na tulioko pembezoni. Tunatumia nguvu na ushawishi wa kisiasa. Tunapata hasara na uharibifu wa ardhi yetu, nyumba na riziki. Sisi ni wawekezaji wenye mitaji ya fedha. Sisi ni washiriki wa kwanza wa majanga na wale wanaoongozana na jamii katika safari ya kupona na ustahimilivu.

2.8 Tunachangia tatizo. Tunachangia katika suluhisho. Sisi ni wa mahali husika na wa kimataifa. Tunaungana na wenzetu, tunabadilishana uzoefu wetu na tunaweza kutumia mitandao yetu na utambulisho wa Anglikana kuhamasisha kuchukua hatua. Hatusemi kutokana na msimamo mmoja tu bali kutokana na misimamo mingi. Hatuzungumzi tu na wengine; tunazungumza pia na sisi wenyewe. Sisi sote ni sehemu ya mtandao wa uumbaji wa Mungu ‘kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana’ (Wakolosai 1:16). Na tumeitwa sasa kutenda pamoja kwa ajili ya binadamu wote, kwa viumbe vyote, na maskani yetu ya pamoja, sayari dunia.

2.9 Kufikia Lambeth Conference ijayo, maeneo mengi ya Ushirika hayatakuwa yanafaa kwa makazi, kwa sababu ya ukame, kupanda kwa vina vya bahari na athari nyingine tunapojaribu kufikia mwisho wa mambo yote katika mabadiliko ya hali ya hewa. Wakati huohuo licha ya hali halisi hii mbaya, uzalishaji wa kaboni unaendelea kuongezeka na kuna zaidi ya migodi mipya 50,000 ya mafuta ghafi unaoendelea.[ii] Bahari na mito yetu imejaa plastiki na watu wanakufa kutokana na hewa iliyochafuliwa. Mtandao wa maisha unakuwa umeharibiwa sana na kupoteza viumbe hai, ikiwa ni pamoja na mazoea ya ukataji miti, uvuvi wa kupitia kiasi na kilimo kisichoendelevu, kiasi kwamba uadilifu wa uumbaji unakuwa kwenye tishio.

2.10 Mwitikio wa ulimwengu umekuwa duni kabisa, katika kiwango cha rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya kushughulikia tatizo na katika kiwango cha uharaka ambacho wale walio na nguvu zaidi ya kufanya mabadiliko makubwa wanachukua hatua.

## 3 Uthibitisho

3.1 Kwa ajili yetu wenyewe na kwa vizazi vijavyo tunahitaji kuchukua hatua sasa, kwa dharura na kasi.

3.2 Hata hivyo, vitendo ni vigumu kudu isipokuwa pia kuwe na mabadiliko ya mioyo na fikra ambayo yataongoza vitendo hivyo. Dharura ya hali ya hewa si tu mgogoro wa kimwili, pia ni mgogoro wa kiroho, ambao unazidishwa na uchoyo, kutojali na ubinafsi.

3.3 Binadamu anahitaji mabadiliko ya kiroho na kiutamaduni. Tunapaswa kuona ulimwengu kwa namna tofauti: kutubu na kukataa mtazamo wa kinyonyaji wa ulimwengu, ambao unaona dunia na asili yote kama kitu cha kutumiwa, na kukumbatia mtazamo wa kimahusiano wa ulimwengu katika moyo wa mafundisho ya Kristo. Hii inaungwa mkono hasa na wazawa katika mazingira ya asili, ambao wanaona hali kubwa ya kutegemeana katika viumbe vyote.

## 4 Maombi Maalum (Miito)

4.1 Tunatoa wito kwetu sisi wenyewe maaskofu na watu wa majimbo yetu, dayosisi na parokia:

4.1.1 Kuenzi uumbaji wa ajabu wa Mungu, tukitambua kutegemeana kwa kina kwa maisha yote duniani na kutubu matendo na theolojia za utawala, ambazo zimesababisha madhara makubwa duniani na dhuluma kwa watu wake.

4.1.2 Kutambua migogoro mitatu ya mazingira kuwa ni mgogoro wa maadili ya kitamaduni na kiroho na kutumia nguvu na ushawishi wa Kanisa kujipatia changamoto sisi wenyewe na binadamu wote kubadilisha mawazo yetu dhidi ya unyonyaji wa ulimwengu wa asili kuwa uhusianio mmoja wapo na uwakili, kama ilivyo hekima ya desturi ya Kikristo na kwa watu wazawa

4.1.3 Jumuisha Alama ya Tano ya Utume katika maisha ya makanisa yetu kwa: kujumuisha Wito huu katika mifumo yetu ya jimbo na parokia; kufundisha watu wetu juu ya masuala ya mazingira; kukumbatia liturujia za uumbaji, na kujibu kwa sala na maombolezo kama vile wakati wa Msimu wa Uumbaji; kupaza sauti za kinabii za vijana na wanawake ambao wanatoa wito wa haki ya hali ya hewa; na kuanzisha ushirikiano wa mshikamano na dayosisi zilizo katika mstari wa mbele wa mabadiliko ya hali ya hewa.

4.1.4 Kuiwezesha jamii kujenga ustahimilivu ili kuwasaidia wahimili na kupona kutokana na majanga, na kukuza sauti ya kinabii ya vijana na jukumu muhimu la wanawake kama walinzi wa dunia, kutambua kwamba mabadiliko ya hali ya hewa huathiri wanawake na vizazi vijavyo.

4.1.5 Kujiunga katika mpango wa Msitu wa Ushirika, kulinda na kurejesha misitu na mazingira mengine katika sayari yetu na kujitolea kukuza upandaji miti wakati wa uthibitisho, na wakati mwingine muhimu wa maisha na imani, kama ishara ya ukomavu wa kiroho.

4.1.6 Kuhakikisha tunatumia na kuwekeza mali zetu kimaadili kuwa habari njema kwa sayari yetu na watu na, kama suala la uharaka, kuondoa fedha zetu kutoka katika uchimbaji wowote mpya wa mafuta, na kutafuta kuwekeza katika vyanzo vya nishati mbadala.

4.1.7 Kutambua athari katika maisha yetu na kujizatiti kufanya mabadiliko katika namna tunavyoishi, kupunguza kusafiri, matumizi ya nishati.

4.2 Tunatoa wito kwa Vyombo vya Ushirika:

4.2.1 Ahadi za usaidizi ili kukabiliana haraka migogoro mitatu ya kimazingira ambayo ni mabadiliko ya hali ya hewa, upotevu wa viumbe hai na uchafuzi wa mazingira, na kusaidia kutoa rasilimali kwa majimbo katika jitihada zao.

4.2.2 Wateteepaze sauti kwa jumuiya ya kimataifa ili kutoa, kama suala la haki, fedha zinazohitajika kwa sababu ya hasara na uharibifu kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, na kuzungumza na kutenda kinabii ndani ya Ushirika juu ya suala hilo, kuonyesha mshikamano.

4.3 Tunatoa wito kwa viongozi wa ulimwengu:

4.3.1 Watekeleze mabadiliko ya sera yaliyo thabiti na ya haraka, ikiwa ni pamoja na:

- kufikia lengo la kutozalisha hewa ya ukaa mapema kadiri iwezekanavyo ili kupunguza kupanda kwa joto la wastani duniani hadi digrii 1.5 juu ya viwango vya kabla ya viwanda.
- kutimiza na kuongeza kwa kiasi kikubwa kutoa fedha kuchangia mabadiliko ya hali ya hewa, ikiwa ni pamoja na kupoteza na uharibifu kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.
- kusimamisha uchimbaji mpya wa gesi na mafuta, wakati huohuo wawezeshe na kufadhili nchi zinazoendelea zikiwa katika wakati wa mpito wa kuwa na nishati safi inayoweza kutumika tena.
- kulinda na kurejesha viumbe hai na kukabiliana na uchafuzi wa mazingira.

4.3.2 Kutoa changamoto kwa mataifa tajiri zaidi na wale walio na jukumu kubwa la mabadiliko ya hali ya hewa kuongoza katika hatua za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na kutoa fedha kwa nchi nyingine ili kupunguza uzalishaji wa hewa chafu.

4.3.3 Kusaidia ushirikiano wa kimataifa na malengo makubwa ya mpito ya kuwa na nishati safi na mbinu za matumizi endelevu ya ardhi na mifumo ya chakula.

4.3.4 Kukubali kwamba kiwango na uharaka wa dharura ya hali ya hewa ni kwamba siasa lazima ziongoze njia ya kuchukua hatua kwa kuzingatia sayansi na kutokana na wito wa kimaadili kutambua kutegemeana kwetu na kila mmoja na dunia ya asili.

4.3.5 Kutambua hekima iliyo ndani ya jamii za imani juu ya thamani na utunzaji wa uumbaji na jukumu ambalo waumini, na viongozi wao wa imani, wanaweza kuleta ili kushawishi mabadiliko katika jamii.

## Melezo ya Mwisho

i. Ripoti ya IPCC 2022 **https://unfccc.int/news/the-evidence-is-clear-the-time-for-action-is-now-we-can-halve-emissions-by-2030**

ii. **https://theconversation.com/how-treaties-protecting-fossil-fuel-investors-could-jeopardize-global-efforts-to-save-the-climate-and-cost-countries-billions-182135**

# B. MAENDELEO ENDELEVU

## 1 Utangulizi

1.1 Mamilioni ya watu leo wanaishi katika jamii na mataifa ambapo umaskini uliokithiri na ukosefu wa usawa huharibu maisha yao na uwezo wa kustawi. Janga la Covid-19 limeongeza ukosefu wa usawa na kudhoofisha mafanikio ya maendeleo ya miongo ya hivi karibuni. Viwango vya umaskini uliokithiri viliongezeka wakati wa janga la ugonjwa, na zaidi ya watu milioni 700 sasa wanakadiriwa kuwa wanaishi chini ya dola 1.90 kwa siku.

1.2 Waanglikana wengi na Wakristo wengine ni miongoni mwa idadi hii. Watu wanakabiliwa na changamoto sugu katika maisha ya kila siku na majanga ya ghafla, mara nyingi yanayohusiana na migogoro, matatizo ya kiuchumi, na mabadiliko ya hali ya hewa na kusababisha ukame, kupanda kwa kina cha bahari, mafuriko na moto. Majanga haya yanaondoa uhai, kuharibu nyumba, uharibifu wa maisha, kusababisha ukosefu wa chakula, kukatiza elimu, kuathiri afya, uhamiaji wa kulazimisha, kuweka watu katika hatari ya kununuliwa kiharamu, kuongeza unyanyasaji wa kijinsia, kuvuruga jamii na kuvunja familia. Yana athari kubwa sana kwa wanawake, vijana na watu wazawa. Athari za majanga haya ni kubwa sana, kifedha na kutokana na hofu inayosababishwa nayo. Janga la Corona lilisababisha hali kuwa mbaya zaidi, kuongezeka kwa umaskini na ukosefu wa usawa, ndani ya nchi na baina ya nchi.

1.3 Hali hii inaweza pia kuonekana kama matokeo ya dhambi ya binadamu, kwa kuwa tumeshindwa kumpenda Mungu, kumpenda jirani yetu na kujali viumbe. Hata hivyo, kama ilivyoelezwa katika 1 Petro, iliyofafanuliwa katika Lambeth Conference 2022, tumeitwa “kuwa na upendo wa kweli” (1 Petro 1:22), unaoonyeshwa kupitia ukarimu, uwakili na huduma ya pamoja (diakonia) (1 Petro 4:9-10). Mambo haya ni muhimu katika kuhudumiana kwetu ndani ya nchi na kimataifa.

1.4 Yesu alituita sote tufuate huduma yake tukitafuta haki na kutoa huduma ya upendo: “kuwahubiria maskini Habari Njema...kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa, na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa.” (Luka 4: 18-19)

## 2 Azimio

2.1 Kama Wakristo, tumaini letu liko kwa Bwana, aliyeumba mbingu na dunia. Tumaini letu linamaanisha kwamba tumeitwa katika tukio la kushiriki katika hadithi ya milele ya Mungu, kutupeleka kuelekea njia ambayo ulimwengu ungepaswa kuwa, unapaswa kuwa na siku moja utakuwa kama Ufalme wa Mungu unaokuja.

2.2 Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDG) ni maono muhimu ya kustawi kwa watu na sayari, kuishi pamoja kwa amani na ustawi na kwa kushirikiana kama binadamu wamoja. Wanadamu wanaitwa kutenda haki, kuonesha huruma na mshikamano na wale ambao ni maskini, waliotengwa, na wanaokabiliwa na dhuluma, pamoja na dhuluma ya kijinsia. SDG hutoa maono na mfumo ambao sisi sote tunaweza kushiriki katika kufanya kazi kuelekea ulimwengu wa haki zaidi, ulimwengu ambao wote wana nafasi ya kustawi na ambapo hakuna mtu anayeachwa nyuma. Kanuni za SDGSzinakisiwa katika Alama Tano za Utume wa Anglikana.

## 3 Uthibitisho

3.1 Kwa nia hii, tuko katika msimu wa kuchukua hatua: fursa muhimu, ya haraka ya kufikiria tena ulimwengu wetu na kushughulikia ukosefu huu wa haki na vitisho. Mwaka 2030 ni tarehe muhimu iliyokusudiwa kufanikisha malengo ya SDG. Kama Waanglikana, utume wa Kanisa, yaani, utume wa Kristo, unaonyeshwa katika Alama zetu Tano za Utume. Hawa wanakumbuka utume wa Yesu wa kuleta habari njema kwa maskini, kufunguliwa kwa walioonewa, utimilifu wa uzima kwa wote na kufanywa upya kwa viumbe vyote (Luka 4:18; Yohana 10:10; Marko 16:15). Ni wito wetu na shauku zetu kufuata nyayo za Yesu. SDGs ni nyenzo ya kusaidia kuhabarisha uelewa na mwitikio wetu, wito wetu kwa vitendo, kuwa sehemu ya harakati pana ya kimataifa kwa watu na sayari. Tumeitwa kuwa Kanisa la Mungu kwa Dunia ya Mungu.

## 4 Maombi Maalum (Miito)

4.1 Tunatoa wito kwetu sisi wenyewe maaskofu na watu wa majimbo yetu, dayosisi na parokia:

4.1.1 Kutekeleza kwa ukamilifu zaidi Alama Tano za Utume katika maisha ya makanisa yetu tunapotumikia kama Kanisa la Mungu kwa Dunia ya Mungu.

4.1.2 Kutambua ni Malengo gani ya Maendeleo Endelevu yana umuhimu zaidi kwa utume wetu na uyaambatishe katika mpango wetu wa utume wa jimbo kwa ajili ya utekelezaji.

4.1.3 Kuyashirikisha na kuyawezesha makanisa yetu kufanya kazi pamoja na majirani zao wa mahali walipo na wa kimataifa kwa ajili ya mabadiliko, kwa kutumia vipawa na mali zetu ili kujenga jamii zenye ustahimilivu, endelevu na za haki kulingana na dira ya Malengo ya Maendeleo Endelevu kama inavyoonekana katika Alama Tano za Utume.

4.1.4 Kusaidiana na kutiana moyo katika Ushirika wote kufanya kazi pamoja ili kufikia utu wa binadamu wote na kustawi (Yohana 10: 10) katika sayari inayostawi.

4.2 Tunatoa wito kwa Vyombo vya Ushirika:

4.2.1 Vishikilie Alama Tano za Utume kuwa sehemu muhimu ya utambulisho wa Anglikana na utume wetu na utume kamili kama Kanisa la Mungu kwa Dunia ya Mungu.

4.2.2 Kuhamasiaha Alama Tano za Utume, ikiwa ni pamoja na dira yake ya kuunda upya ulimwengu wetu, kushughulikia hitaji la binadamu kwa huduma ya upendo, kupinga mifumo ya jamii isiyo ya haki na kulinda uumbaji, na hivyo kuhimiza na kuandaa Ushirika kutoa mchango mkubwa katika kufikia matarajio ya Malengo ya Maendeleo Endelevu. [Lugha imebadilishwa kutoka kuwa dhana ya 'kampeni' ya kimataifa na kukita zaidi katika utekelezaji katika dayosisi]

4.2.3 Vishirikiane kwa kushirikiana na jumuiya nyingine za imani na watu wote, kwa ajili ya ustawi wa pamoja wa watu na sayari. Hasa, kusaidia michango ya wanawake na vijana na kukuza sauti zao.

4.2.4 Vitoe changamoto kwa miundo isiyo ya haki ambayo inaendeleza mifumo ya kiuchumi na kisiasa inayoendesha ukosefu wa haki, ukosefu wa usawa na ukosefu wa utulivu ndani na baina ya nchi.

4.3 Tunatoa wito kwa viongozi wa ulimwengu:

4.3.1 Wajitolee kutoa fedha na kuchukua hatua ili kuwezesha mataifa yote ya ulimwengu yaweze kutimiza Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030, pamoja na dira yake ya 'kutoacha mtu nyuma'.

4.3.2 Kutambua umuhimu wa kimkakati wa watendaji wa imani na mashirika ya imani na kuwajumuisha kama washirika muhimu katika maendeleo endelevu na hali ya utayari wakati wa maafa, ustahimilivu na kuchukua hatua.

## 5 Utekelezaji

Maaskofu wanaalikwa kufuatilia miito hiyo katika ngazi ya jimbo, katika sinodi na mikusanyiko ya jimbo, ili kuifanya iwe hati hai, wakiijumuisha kuwa vipaumbele katika upangaji na utekelezaji wa utume.

Miito hii inawataka maaskofu kuonyesha uongozi na kuitekeleza ndani ya majimbo na dayosisi zao, kwa msaada wa Vyombo vya Ushirika pamoja na mashirika ya utume na maendeleo. ACC na Kamati yake ya Kudumu itafuatilia wito maalumu na kuripoti juu ya maendeleo hadi mwaka 2030, ikiwa ni pamoja na katika ACC19. Vyombo vya ngazi ya Ushirika, ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Anglikana katika Umoja wa Mataifa, Muungano wa Anglikana, idara za ACO kama vile Jinsia, na Mitandao, Tume na mashirika husika ya Anglikana yote yatashirikiana kusaidia kuunganisha, kuandaa na kuhamasisha Makanisa Wanachama, pia kufanya kazi na mashirika ya kimataifa, katika kutimiza hatua zilizowekwa katika Wito huu wa Mazingira na Maendeleo Endelevu

# WITO WA LAMBETH
# UTAMBULISHO WA ANGLIKANA

*"...ninyi ni uzao teule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu."*

## 1 Azimio

1.1 Kanisa ni jumuiya ya Kristo aliyefufuka. Wakristo wanakiri kwamba Kanisa la Kristo ni moja, takatifu, pana, na la kitume.[i] Kanisa ni tunda la utume wa ukombozi wa Mungu kupitia Neno lililofanyika mwili (Rum. 12:5; Gal. 3:26-28). Kanisa liko hai katika utambuzi wake wa utume wa Mungu na katika kushiriki wake katika utume wa Mungu.

## 2 Uthibitisho

2.1 Mapokeo ya Kianglikana yana mizizi yake katika historia ya pamoja na ukatoliki, mabadiliko, utume wa kimataifa, na ushuhuda wa tamaduni mbalimbali. Umoja wetu, na matumaini ya umoja wa kina wa Kikristo, huonyeshwa katika Matamko Manne ya Chicago-Lambeth:

i. Maandiko Matakatifu ya Agano la Kale na Agano Jipya, kuwa "yanajumuisha mambo yote ya lazima kwa ajili ya wokovu," na kuwa ni kanuni na kiwango cha mwisho cha imani.

ii. Imani ya Mitume, kuwa ni Ishara ya Ubatizo; na Imani wa Nisea, kuwa ni tamko toshelevu la imani ya Kikristo.

iii. Sakramenti mbili zilizoamriwa na Kristo mwenyewe: Ubatizo na Meza ya Bwana inayotolewa kwa matumizi yasiyokoma ya maneno ya Kristo ya Taasisi, na ya mambo yaliyoamriwa naye.

iv. Maaskofu wa Kihistoria, ikitumiwa mahali husika katika utaratibu wa uendeshaji wake kulingana na mahitaji mbalimbali ya mataifa na watu walioitwa na Mungu katika Umoja wa Kanisa Lake.[ii]

2.2 Msingi katika maandiko, na kuongozwa na mapokeo na sababu. Waanglikana wanatafuta kuwa waaminifu kwa Mungu katika utamaduni anuwai na katika hali anuwai za binadamu. Katika ushirika na Kanisa la Canterbury, Ushirika wa Anglikana umekua na kuwa familia ya makanisa na majimbo yanayotegemeana katika nchi zaidi ya 165.

2.3 Kwa hivyo, Waanglikana, wanaamini mfumo wa kanisa unaoonekana na wa kitaasisi.[iii] Kila jimbo la Ushirika wa Anglikana ni huru na linaitwa kuishi kwa kutegemeana. Mihimili Minne ya Ushirika imeanzishwa ili kuonyesha kutegemeana kwa Anglikana.[iv] Mihimili hii ni:

i. Askofu Mkuu wa Canterbury

ii. Lambeth Conference

iii. Baraza la Ushauri la Anglikana, na

iv. Mkutano wa Maaskofu.

Makanisa Wanachama wa Ushirika wa Anglikana hufasiliwa kwa kuhusiana na ushirika wao na wao kwa wao na kwa Mihimili ya Ushirika.

2.4 Ubatizo wetu wa pamoja unawaita watu wote wa Mungu kwenye maisha ya huduma katika utumishi wa Bwana Yesu Kristo. Tunathibitisha huduma ya pampja iliyowekwa wakfu kulingana na utaratibu wa aina tatu wa mashemasi, makasisi (wapresbiteri), na maaskofu. Tukiundwa katika jumuiya ya kiliturujia, tukilishwa na Neno na sakramenti, tunageuka kuwa mashahidi wa Ubwana wa Kristo ulimwenguni.[v]

2.5 Ushuhuda wetu umetokana na jamii za mahali husika na unafika ulimwenguni kote. Wito wa utume umeelezwa katika Alama Tano za Utume wa Anglikana.[vi] Utume wa Kanisa ni utume wa Kristo:

i. Kutangaza Habari Njema za Ufalme
ii. Kufundisha, kubatiza na kulea waumini wapya
iii. Kushughulikia mahitaji ya binadamu kwa huduma ya upendo
iv. Kubadili mifumo ya kijamii isiyo ya haki, kupinga vurugu za kila aina na kutafuta amani na maridhiano;
v. Kujitahidi kulinda uadilifu wa uumbaji, na kuendeleza na kufanya upya maisha ya dunia.

**3 Maombi Maalum (Miito)**

Maaskofu waliokusanyika katika Lambeth Conference 2022 wanatoa wito kwa Ushirika:

3.1 *Kufikiria upya maono na zoezi la Ushirika*

Kufahamu kwamba desturi za pamoja zinaweza kuhafifisha mtazamo wetu kuhusu dunia, kwamba kipawa cha taasisi kinaweza kulisha taasisi, kwamba kipawa cha mamlaka kinaweza kuharibiwa na matumizi mabaya ya mamlaka, na kwamba neema inayopatikana katika utambuzi katikati ya kutokubaliana inaweza kuharibiwa na ubaguzi, tunatamani kuwa na dira mapya ya Ushirika. Tunatoa wito kwa Askofu Mkuu wa Canterbury na Baraza la Ushauri la Anglikana kuanzisha kikundi huru cha utafiti ili kuelewa namna mbalimbali ambazo Ushirika (koinonia) unaeleweka na kujumuishwa katika majimbo na mapokeo ya kikanisa.[vii] Kikundi hiki cha utafiti baina ya tamaduni mbalimbali kitatoa rasilimali ambazo zitajenga upya, kuhamasisha, na kufanya upya theolojia za Ushirika na njia za kuwa katika Ushirika. Muundo wa awali wa utafiti huu (kwa mfano, kufafanua, mbinu, upeo, na matokeo) utawasilishwa kwa kamati ya kudumu ya ACC mwaka 2024. Kikundi hiki cha utafiti kitachapisha seti yake ya kwanza ya nyenzo mwaka 2025.

3.2 *Kuangalia Uwezekano wa Mikutano ya Kimataifa na ya Kitamaduni katika Eneo la Kusini mwa Ulimwengu*

Hii ni zama ambayo inatawaliwa na utawala wa kimabavu, mazingira magumu na harakati za watu wazawa; ushirikiano na migogoro ya kidini; uhamiaji wa watu wengi; kushikilia nafasi nyingi; mgogoro wa hali ya hewa; na mabadiliko makubwa katika sayansi na teknolojia. Katikati ya changamoto na fursa hizi, na katika tamaduni tofauti na anuwai ambazo zinaunda Ushirika wetu, tunasherehekea uwepo wa Kristo aliyefufuka ulimwenguni na kushuhudia tumaini linalopatikana katika Injili. Kwa kuzipa kipaumbele sauti za viongozi wazawa, wanawake, vijana, na walei, tunatoa wito kwa familia pana ya Kianglikana kukusanyika pamoja katika ushuhuda wa furaha kwa maneno mazuri ya Injili katika tamaduni zetu nyingi zilizoonyeshwa katika sanaa za kuona, fasihi na sanaa za maonyesho.[viii] Kufurahia huku kwa tamaduni mbalimbali kutatoa njia mpya ya kupambanua Roho Mtakatifu na hivyo kwa Kanisa kufanya upya maono yake na utendaji wa utume wa Kikristo.

Tunatoa wito kwa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Ushauri la Anglikana kuanzisha kikundi cha uchunguzi ili kuwasilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya tamasha au kongamano hili la kimataifa la Anglikana.[ix] Ripoti ya awali, inayoweka mfumo wa marejeleo kwa ajili ya upembuzi yakinifu, inapaswa kuwasilishwa na Katibu Mkuu kwa kamati ya kudumu ya ACC mwaka 2025. Uchunguzi yakinifu wa mwisho unapaswa kuwasilishwa na kikundi cha uchunguzi kwenye ACC-19 mwaka 2026. Ikiwa inafaa, Katibu Mkuu, kwa kushauriana na Askofu Mkuu wa Canterbury, ataitisha mkutano wa kimataifa wa Anglikana na kuunda kikundi cha maandalizi. Mkutano huu wa kimataifa utafanyika kabla ya Lambeth Conference.

3.3 *Kutathmini Vyombo vya Ushirika*

Tunatoa wito wa kufanya tathmini ya Vyombo vya sasa vya Ushirika. Tunamwomba Askofu Mkuu wa Canterbury aanzishe kikundi huru cha tathmini kuhusu Vyombo vya Ushirika huku mkazo maalumu ukiwekwa kwenye jinsi utaratibu wote wa utumishi (pamoja na walei) unavyohusiana na Vyombo na/au unavowakilishwa katika Vyombo hivyo. Ni kwa kiwango gani vyombo hivi vinafaa kusudi? Je, ni kwa kiasi gani baadhi (au vyote) ya Vyombo vinaweza kubadilishwa ili kutumika katika Ushirika wa leo na baadaye? Je, kunapaswa kuwa na Chombo zaidi cha Ushirika ili kuweza kupaza sauti za wale ambao mara nyingi watanategwa, viongozi wazawa, walei wanawake na vjina?[x] Tathmini hii inapaswa kuwasilishwa kwenye ACC-19 katika mkutano wake mwaka 2026.

3.4 *Kuhuisha Kujizatiti kwa Anglikana kwenye Alama Tano za Utume*

Tunatoa wito kwa maaskofu wote kuongoza dayosisi zao zijizatiti tena na kuthibitisha tena Alama Tano za Utume.[xi] Kamati ya Kudumu ya Baraza la Ushauri la Anglikana, kwa kushauriana na mitandao na idara husika za Jumuiya, zipewe jukumu la kuitisha kikundi cha kimataifa cha wataalamu wa utume wa Kianglikana ili kuchunguza njia anuwai ambazo uthibitishaji huu tena na kujizatiti tena katika utume umejumuishwa katika Ushirika wote. Utafiti huu utachapishwa mwishoni mwa mwaka 2026 kama dira mpya ya utume katika Ushirika.[xii]

## Melezo ya Mwisho

i. Imani ya Nisea: Tume ya Kudumu ya Jumuiya yote ya Anglikana juu ya Umoja, Imani na Utaratibu (IASCUFO), *Kuelekea Mkutano wa Vyombo: Mazingatio ya Kihistoria na Kiteolojia ya Vyombo vya Ushirika wa Anglikana* (2018), 1-2.

ii. Lambeth Conference 1888, Azimio la 11. Tazama pia maumbo yaliyowekwa katika Kitabu cha Maombi ya Pamoja (1662).

iii. Makala XIX–XXI, *Kitabu cha Maombi ya Pamoja* (1662). Tazama pia "Kanuni za Utaratibu wa Kanisa" zilizowekwa katika Barua ya 1.5 (Lambeth Conference, 1878): **https://www.anglicancommunion.org/resources/document-library/lambeth-conference/1878/recommendation-1-union-among-the-churches-of-the-anglican-communion-encyclical-letter-15?language=english&year=1878**, ilipatikana Julai 1, 2022.

iv. *Kuelekea Mkutano wa Vyombo* (2018).

v. Angalia Mashauriano ya Kimataifa ya Kilitrujia ya Anglikana (IALC), *Ripoti kuhusu Uundajiwa Kilitrujia wa Wote Waliobatizwa* (2021): **https://www.anglicancommunion.org/media/493609/The-Liturgical-Formation-of-All-the-Baptised_ACC18_IALC_2301.pdf**.

vi. Tazama **https://www.anglicancommunion.org/mission/marks-of-mission.aspx**. Alama za Utume zilianza kujitokeza katika Baraza la Ushauri la Anglikana (ACC-6) huko Badagry, Nigeria (1984). Lambeth Conference ya 1988 ilithibitisha dhana hii iliyoibuka ya utume wa Kianglikana ("Asili na Maana ya Utume") na katika ACC-8 mwaka 1990 alama ya tano katika kushughulikia mgogoro wa ikolojia iliongezwa. Lambeth Conference 1998 uliidhinisha Alama Tano za Utume. Angalia Cathy Ross, "Utume" katika Mark D. Chapman, Sathianathan Clarke na Martyn Percy eds. *The Oxford Handbook of Anglican Studies* (Oxford, 2015), 504-515; Robert S. Heaney na John Kafwanka K, "Utume katika Utume wa Mungu" katika Robert S. Heaney, John Kafwanka K, na Hilda Kabia, *Kanisa la Mungu kwa Dunia ya Mungu* (New York Church Publishing, 2020), 1–19.

vii. *1 Kor.* 10:16-17.

viii. **Ka Hao - Kusifu Ndicho Ninachofanya - YouTube** Huu ni mfano wa jinsi vijana katika Jimbo moja wameshughulikia utambulisho wao wa asili na wa Kikristo kupitia mbinu shirikishi ambayo inachukulia kwa uzito Injili kuhusiana na hali ya uzawa na mchakato wa ubunifu. (Wimbo) huu wa *Waiata* ni matokeo ya jitihada za kiroho, kitheolojia, na kisanii. Zaidi ya hayo, utendaji wenyewe ni kitendo cha utambuzi wa kiteolojia na kiroho. Udhihirishaji huo wa kisanii na kiteolojia, kwa sehemu, ni yale tunayoyaona kama kazi na ushahidi wa mkutano wa kimataifa na wa kiutamaduni.

ix. Mkutano wa kimataifa kama huo unaweza kupata msukumo katika Mabaraza ya Anglikana yaliyokutana London, Uingereza mwaka 1908; Minneapolis, Marekani mwaka 1954; na Toronto, Canada mwaka 1963. Kwa habari juu ya Kongresi ya mwisho ya Anglikana huko Toronto, Canada (1963) angalia: **https://www.episcopalarchives.org/e-archives/the_witness/pdf/1963_Watermarked/Witness_19630905.pdf**.

x. Mnamo Mei 2, 2022 Askofu Mkuu wa Canterbury aliahidi watu wa Mataifa ya Kwanza ya Kanada majadiliano kuhusu haki za watu wa Asili. Tazama Askofu Mkuu wa Canterbury, "Msamaha kwa Watu wa Asili wa Kanada" (Taarifa kwa Vyombo vya Habari, Mei 2, 2022): **https://www.archbishopofcanterbury.org/speaking-writing/speeches/read-archbishop-justins-apology-indigenous-peoples-canada**, ilipatikana Juni 23, 2022.

xi. Angalia pia Wito wa Lambeth kuhusu Utume na Uinjilisti.

xii. Ikiwa inaamuliwa kuwa mkutano wa kimataifa na wa kitamaduni unafanyika, uchunguzi na tafiti zilizotajwa katika Wito huu zitakuwa nyaraka muhimu katika kuunda mkutano huo.

# WITO WA LAMBETH
# KANISA SALAMA

## 1 Utangulizi

Ujumbe wa Lambeth Conference ulikuwa Kanisa la Mungu kwa Dunia ya Mungu na maaskofu walijifunza 1 Petro. Katika barua hii, mtume Petro aliandika kwa Wakristo waliotawanyika kote Asia Ndogo akiwakumbusha utambulisho wao katika Kristo kama watu wateule wa Mungu, waliotakaswa na Roho kwa ajili ya utii kwa Yesu Kristo (1 Petro 1.1-2). Agano la Kale na Agano Jipya zinaonyesha wito wa kuwa mtakatifu kama mwitikio sahihi wa neema ya Mungu (1 Petro 1.15-16). Kwa hiyo Wakristo wanapaswa kuishi kama watumishi wa Mungu na wanapaswa kumheshimu kila mmoja na kuipenda familia ya waumini (1 Petro 2:6-17). Viongozi wa Kikristo wameitwa kulinda watu wa Mungu wanaowahudumia (1 Petro 5.1-2).

## 2 Azimio

2.1 Katika kutoa wito huu tunazingatia sana, na kuongozwa na:

- sauti za wale ambao wamepitia unyanyasaji katika muktadha wa kanisa;
- hali mbalimbali ambazo zinaweza kuwafanya watu au jamii kuwa katika hatari zaidi ya vurugu, unyanyasaji na kutengwa kama vile rangi, jinsia, mwelekeo wa kijinsia, ukabila, imani ya kidini, wanaoishi na ulemavu wa kimwili, ulemavu wa akili, au mazingira magumu ya kiuchumi;
- shirika la Afya Duniani linatoa nukuu ya utafiti unaokadiria kuwa:
  - duniani kote, hadi watoto bilioni 1 wenye umri wa miaka 2–17 walifanyiwa unyanyasaji wa kimwili, kingono, au kihisia (unyanyasaji) au kutelekezwa katika mwaka uliopita. Ukatili dhidi ya watoto una athari za kudumu juu ya afya na ustawi wao[i];
  - Mwanamke 1 kati ya 3 ulimwenguni kote amekabiliwa na unyanyasaji wa kimwili na/au wa kingono kutoka kwa mwenzi au unyanyasaji usio wa wenzi katika maisha yao. Vurugu hii inaweza kusababisha madhara makubwa ya kiafya ya muda mfupi na ya muda mrefu vilevile gharama za kijamii na kiuchumi kwa wanawake, familia zao na jamii[ii];
- Ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu (SDG), ni:
  - “kuondoa aina zote za ukatili dhidi ya wanawake na wasichana katika nyanja za umma na binafsi, ikiwa ni pamoja na biashara haramu ya kusafirisha binadamu, ngono na aina nyingine za unyonyaji” (Lengo la 5.2);
  - “kukomesha dhuluma, unyonyaji, biashara haramu ya binadamu na aina zote za ukatili dhidi ya wanawake, watoto na mateso ya watoto,” (lengo la 16.2).[iii]

2.2 Tunatoa wito huu tukijua kabisa kushindwa kwa ulinzi/Kanisa Salama katika taasisi za kidini ikiwa ni pamoja na makanisa ya Ushirika wa Anglikana, kama ilivyoonyeshwa na hoja za serikali, kesi zilizoripotiwa na vyombo vya habari. Kuna watu wanaofanya kazi ndani ya taasisi za kidini, makasisi pamoja na walei, ambao wamesaliti uaminifu na kunyanyasa watoto na watu wazima ambao walikuwa na wajibu wa kichungaji. Kuna viongozi wa dini ambao wamekataa au kupunguza uzito wa unyanyasaji huu na unyanyasaji. Taasisi za kidini zimeongeza athari za unyanyasaji wa awali kwa kushindwa kushughulikia kwa ufanisi. Wameshindwa kuchukulia ufichuzi kwa uzito, kuripoti unyanyasaji haraka kwa mamlaka husika, kumwajibisha mhalifu na/au kuendelea kutoa huduma ya kichungaji kwa wale ambao wamedhulumiwa. Kwa sababu hiyo, sifa ya uwazi, uwajibikaji na imani ya umma katika taasisi nyingi za kidini umeharibika.

2.3 Tunatangaza:

- ushuhuda wa Maandiko kwa upendo wa Mungu kwa wanadamu wote na kipaumbele kilichowekwa katika huduma ya Yesu kwa watoto, walio katika mazingira magumu na waliotengwa;
- umuhimu unaoendelea wa tafakari ya Lambeth Conference 2008 juu ya aina nyingi za matumizi mabaya ya madaraka katika jamii na Kanisa ambamo wanawake na wasichana wanateseka vibaya. Vurugu zilizofanyika kwa wanawake na watoto katika mwili wa Kristo ni vurugu inayofanywa kwa mwili wa Kristo. Vurugu inakuwa na aina nyingi ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kimwili, kifedha, kihisia, kisaikolojia, kiakili, kitamaduni, kingono na kiroho;
- kwamba tutatimiza Mkataba wa Usalama wa Watu ndani ya Makanisa ya Ushirika wa Anglikana uliopitishwa na Baraza la Ushauri la Anglikana mwaka 2012 (katika ACC-15). Tutatimiza ahadi zake tano za kutoa usaidizi pale ambapo kuna unyanyasaji; kutekeleza ushughulikiaji wenye ufanisi kwenye unyanyasaji; kupitisha na kuhamasisha viwango vya utendaji wa huduma; kutathmini ufaafu wa huduma; na kuhimiza utamaduni wa usalama;
- kwamba tutatekeleza Itifaki ya kutoa taarifa za kufaa kwa huduma kati ya makanisa ya Ushirika wa Anglikana iliyokaribishwa na Baraza la Ushauri la Anglikana mnamo 2016 (katika ACC-16). Tutatekeleza Itifaki hii kwa kuwa na mifumo ya kutoa na kutathmini taarifa wakati wafanyakazi wa kanisa wanapohamia kati ya/ndani ya majimbo;
- kwamba tutafuata Miongozo ya kuimarisha usalama wa watu wote, hasa watoto, vijana na watu wazima walio hatarini, ndani ya majimbo ya Ushirika wa Anglikana yaliyopitishwa na Baraza la Ushauri la Anglikana mwaka 2019 (katika ACC-17). Tutafuata Miongozo hii kwa kuweka mifumo katika makanisa yetu ili kuzuia unyanyasaji na kutoa msaada unaofaa wa kichungaji kwa wale waliodhulumiwa;
- kwamba tutafanya kazi na Tume ya Kanisa Salama ya Ushirika wa Anglikana ambayo mwendelezo wake uliombwa na Baraza la Ushauri la Anglikana mwaka 2019 (katika ACC-17). Tutashirikiana na Tume inapotoa msaada, na kutoa ripoti juu ya maendeleo, ili kuboresha usalama wa watu wote katika makanisa ya Ushirika wa Anglikana.

## 3 Uthibitisho

3.1 Tunakiri kwa aibu kubwa kwamba baadhi ya watu wanaofanya kazi ndani ya Kanisa, makasisi na walei, wamejihusisha na tabia za dhambi, na hata uhalifu, kwa kuwanyanyasa wale wanaowahudumia. Tunaomba msamaha kwa wale ambao wamedhulumiwa na kuumizwa na ambao wanaendelea kuishi na athari za madhara hayo. Tunasikitika sana kwa kushindwa kwa makanisa yetu kuzuia madhara, na kuwasikiliza na kuwasaidia wale ambao wamenyanyaswa. Tunakubali kwamba toba yetu lazima ionyeshwe kwa hatua ya makusudi ya kuimarisha usalama wa jumuiya na taasisi zetu za kanisa.

3.2 Tunathibitisha kuwa:

- sehemu muhimu ya utume wa Kanisa na uanafunzi wa watu wa Mungu ni kujenga jumuiya ambamo watu wote wako salama na wanatunzwa. Imani hii inapaswa iwe sehemu ya msingi ya teolojia yetu na kwa hivyo lazima iwe na utambulisho, mawazo, maneno na matendo yetu katika kuwa Kanisa la Mungu kwa Duania ya Mungu.
- tutachukua hatua ya kufanya makanisa ya Ushirika wa Anglikana kuwa sehemu za usalama ulioimarishwa kwa kila mtu, ambapo wafanyakazi wa kanisa hufanya kazi kwa uadilifu; waathiriwa wa unyanyasaji wanapata huduma na matokeo ya haki; wafanyakazi wa kanisa wanaofanya matendo ya unyanyasaji wanawajibika; na viongozi wa kanisa hawafichi vitendo vya unyanyasaji;

**4 Maombi Maalum (Miito)**

Sisi, maaskofu tuliokusanyika katika Lambeth Conference, tunatoa wito ufuatao:

4.1 sisi wenyewe kama maaskofu, kutimiza wajibu wetu wa kuwalinda watu wote tunaowahudumiwa kwa:

- kuhakikisha sisi wenyewe tunakuwa na maarifa, uelewa, huruma na utambuzi unaohitajika kupitia mafunzo, kusikiliza uzoefu wa wale ambao wamepitia unyanyasaji na kuendelea kushiriki na maaskofu wenzetu;
- kutumia Mkataba wa Usalama wa Watu ndani ya Makanisa ya Ushirika wa Anglikana;
- kutekeleza Itifaki ya kutoa taarifa za kufaa kwa huduma;
- kufuata Miongozo ya kuimarisha usalama wa watu wote, hasa watoto, vijana na watu wazima walio katika mazingira hatari, ndani ya majimbo ya Ushirika wa Anglikana;
- kuhakikisha kuwa kila dayosisi inaweka muundo/mfumo salama wa Kanisa, unaofaa kwa muktadha na rasilimali za mahali husika, kama jambo la dharura;
- kutimiza mahitaji yote ya kisheria katika nchi zetu kuripoti unyanyasaji wa watoto kwa mamlaka na huduma husika;
- kutetea mabadiliko katika sheria na utendaji ndani ya mashirika ya serikali ili kuongeza ulinzi wa watoto, vijana na watu wazima walio katika mazingira hatari.

Kwa kufanya hivyo, tunakiri kwamba maendeleo yetu ni tofauti katika sehemu tofauti za Ushirika, na kwamba baadhi ya majimbo na dayosisi zetu zinakabiliwa na hali kama vile vita na majanga ya asili ambayo husababisha changamoto za kipekee kwa kazi hii;

4.2 kwa Vyombo vya Ushirika, kufanya usalama wa watu wote katika majimbo ya Ushirika wa Anglikana kuwa kipaumbele cha mkazo wao, ugawaji wa rasilimali na uchukuaji hatua;

4.3 kwa watu wa majimbo na dayosisi zetu, kushirikiana nasi kumlinda kila mtu katika jumuiya zetu za kanisa na taasisi kwa kuwa na mifumo, mafunzo na watu katika nafasi ya kuzuia unyanyasaji na kutoa msaada sahihi wa kichungaji kwa wale ambao wamekuwa wakinyanyaswa;

4.4 kwa viongozi wa dunia, kuchukua hatua zozote ambazo ni muhimu ili kufikia malengo ya SDG namba 5.2 na 16.2 (kama ilivyo hapo juu).

Tunatekeleza kupitia wawakilishi wetu kuripoti mara kwa mara kwa Vyombo vya Ushirika kuhusu maendeleo katika kutimiza jukumu letu la kulinda watu wote tunaowahudumia.

## Melezo ya Mwisho

i. Shirika la Afya Duniani, Karatasi ya ukweli, Ukatili dhidi ya watoto, tarehe 29 Novemba 2022 **Ukatili dhidi ya watoto (who.int)**.

ii. Shirika la Afya Duniani, Karatasi ya ukweli, Ukatili dhidi ya wanawake, tarehe 9 Machi 2021, **Ukatili dhidi ya wanawake (who.int)**

iii. Agenda ya mwaka 2030 ya Maendeleo Endelevu ilizinduliwa na Umoja wa Mataifa mnamo Septemba 2015 na inalenga kukomesha umaskini katika aina zake zote. Ina malengo 17 ya maendeleo endelevu na makusudi 169.

# WITO WA LAMBETH
# SAYANSI NA IMANI

## 1 Utangulizi

1.1 Ulimwengu unakabiliwa na hatari nyingi katika muongo ujao kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na upotevu wa bioanuwai, umaskini, magonjwa, vita, njaa na matumizi ya bila kujali ya teknolojia mpya. Katika Wito kufuatia mkutano wa maaskofu katika Lambeth Conference wanakaribisha kila Kanisa la Ushirika wa Anglikana kutambua ndani ya sayansi, nyenzo alizotoa Mungu kwa ajili ya maisha ya imani na kutoa hekima ya imani katika kazi ya sayansi. Tunatoa wito kwa Makanisa yetu yafanye jambo hili kuwa kipaumbele na kusaidia na kuandaa viongozi wa kanisa na wanasayansi kwa kushirikiana kwa ajili ya uongozi huo wa uthubutu na ujasiri.

1.2 Maaskofu wanatoa Wito huu kwa sababu kifungu cha Biblia ambacho wamekuwa wakijifunza wakati wote wa Mkutano, 1 Petro, kinawataka watu wa Mungu kuwa “mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu” na “kutumikiana kwa karama yoyote ile ambayo kila mmoja wenu ameipokea.” (1 Petro 4.10) Kuna wanasayansi wengi wenye uzoefu katika Makanisa yetu duniani kote, Waanglikana ambao wana vipawa vya sayansi kulipatia kanisa na ulimwengu; zaidi ya hayo wanasayansi wengi hutazama hekima ya imani na, hasa, hekima ya Ukristo ili wafahamu udhihirishaji wa neema mbalimbali za Mungu. Pia, 1 Petro anatoa wito si tu kushiriki karama hizi bali ‘kwa nguvu anazojaliwa na Mungu’ (1 Petro 4.11). Kwa maneno mengine, wanasayansi wa Kianglikana na viongozi wa kanisa wanapaswa kujua kwamba hawako peke yao lakini wanaweza kumtegemea yule ambaye kwa nguvu zake wanaishi na kutembea na kuwa na utu wao.

## 2 Azimio

2.1 Licha ya wito kutoka katika mikutano ya Lambeth Conference iliyofuatana hadi Ushirika wa Kanisa kujihusisha na sayansi na teknolojia [i] na kazi ya hivi karibuni ya ECLAS [ii], mtazamo wa pengo kati ya sayansi na imani umeenea zaidi na unaonyeshwa kwa namna tofauti katika sehemu tofauti za Ushirika. Mara nyingi wanasayansi hawajathibitishwa katika kazi yao kuwa wanafunzi na viongozi wa kanisa hawajawa na ujasiri katika kuleta hekima ya imani katika maswali ya kisayansi.

2.2 Kama Askofu Mkuu wa Canterbury alivyosema hivi karibuni, ‘uhusiano kati ya sayansi na imani hutuwasilisha katika njia halisi sana na yenye nguvu ya mabadiliko ya kudumu, mabadiliko makubwa. Kuenea kwetu Duniani [kama Ushirika wa Anglikana], kujitolea kwetu kwa jamii na tumaini letu pamoja na maarifa na utaalamu wa sayansi kunaweza kuunda muungano wenye nguvu’.[iii]

2.3 Aidha, Papa Francis na muungano wa viongozi 40 wa imani duniani walitoa wito wenye nguvu mwezi Oktoba, 2021: “Imani na sayansi ni nguzo muhimu za ustaarabu wa binadamu, zikiwa na kanuni za pamoja na ukamilisho.... Lazima tushughulikie [changamoto tunazokabiliana nazo] kwa kutumia maarifa ya sayansi na hekima ya dini: kujua zaidi na kujali zaidi’.[iv]

## 3 Uthibitisho

3.1 Kama maaskofu tunaamini kwamba mtazamo wa ufa uliopo kati ya sayansi na imani unapaswa kuondolewa katika kila sehemu ya Ushirika wetu wa Anglikana katika muongo ujao muhimu, ili kutimiza wito wetu wa kuwa Kanisa la Mungu kwa Dunia ya Mungu katika kizazi hiki.[v]

3.2 Uhusiano huu wa imani na sayansi unaweza kutokea tu kwa ushirikiano kati ya wanasayansi, wanatheolojia na viongozi wa Kanisa na kati ya Makanisa tofauti ya Ushirika, wakitambua historia ngumu ambayo sayansi imetekeleza katika nchi nyingi na kutumia mbinu za kiteolojia za Anglikana (kutoka katika Maandiko, mantiki na mapokeo) ili kupata ufafanuzi zaidi juu ya uhusiano wa imani ya Kikristo na sayansi.

Kwa hivyo,

3.3 Sisi maaskofu tuliokusanyika kwa ajili ya Lambeth Conference tunajizatiti kukaribisha na kuingia katika mazungumzo ya kitheolojia na sayansi, tukitambua jinsi inavyoeleweka katika maeneo mbalimbali ya Ushirika, tukitambua ndani yake rasilimali zilizotolewa na Mungu kwa ajili ya maisha ya imani na kutoa hekima ya imani ya Kikristo kwa kazi yake hasa kwa maadili ya matumizi yake na matokeo yasiyo na usawa duniani kote.

3.4 Tunatoa wito kwa Makanisa yetu kufanya kazi na washirika na serikali zetu za kiekumeni na kidini (panapowezekana) kutoa kipaumbele cha juu na kusaidia na kuwaandaa viongozi wa kanisa na wanasayansi kwa kushirikiana na viongozi kama hao wenye ujasiri na kujiamini wakitumia ushirikiano ambao tayari unafanyika kupitia Tume, Mitandao na mawakala wengine katika Ushirika wa Anglikana na katika makanisa mengine.

**4 Maombi Maalum (Miito)**

4.1 Tunatoa wito kwa Waanglikana wote wanaposhiriki katika utume kuingia katika mazungumzo ya kitheolojia na sayansi, wakijua jinsi inavyoeleweka katika maeneo mbalimbali ya Ushirika, wakijua ndani yake rasilimali zilizotolewa na Mungu kwa ajili ya maisha ya imani na kutoa hekima ya mbinu ya kitheolojia ya Anglikana (kutoka katika Maandiko, mantiki na mapokeo) kwa kazi yake hasa kwa maadili ya matumizi yake na matokeo yasiyo sawa duniani kote. Kutumia Alama Tano za Utume kama mfumo, hii inaweza kutokea kwa njia zifuatazo:

- *Kutangaza habari njema ya ufalme:* kwa kutambua ndani ya sayansi rasilimali alizotoa Mungu kwa ajili ya maisha ya imani, na hivyo kuiondoa kama kizuizi cha kutangaza injili na imani; kwa kunufaika na sayansi kama hamasa kwa ajili ya ibada yetu kwa sifa na utukufu wa Mungu;
- *Kufundisha, kubatiza na kuwalea waamini wapya:* kwa kutafuta misingi ndani ya sayansi kwa ajili ya imani ya Kikristo na kwa kuthibitisha utu na thamani ya waamini wapya ambao wana asili na kazi za kisayansi;
- *Kushughulikia mahitaji ya binadamu kwa huduma ya upendo:* kwa kutumia rasilimali za sayansi katika masuala yanayotokana na huduma ya afya ya kimwili na ya akili katika kupata huduma ya maji na usalama wa chakula;
- *Kubadilisha mifumo ya kijamii isiyo ya haki, kujaribu kuzuia vurugu za kila aina na kutafuta amani na maridhiano:* kwa kutambua jinsi sayansi inavyoweza kuchangia kukosekana kwa usawa na migogoro, kuzungumzia masuala hayo kutoka kwa mtazamo wa maarifa thabiti ya kisayansi, kutoa maadili na hekima ya imani kwa kutumia teknolojia mpya kama vile AI, vinasaba na teknolojia ya nyuklia;
- *Kujitahidi kulinda uadilifu wa viumbe, kudumisha na kuendeleza uhai wa dunia:* kwa kuchangia hamasa ya theolojia ya Kikristo kwa kuitunza dunia ya kawaida na kuitikia mamlaka ya kimaadili kudhibiti uchu na kutumia uumbaji wa Mungu kwa kujali.

4.2 Tunakaribisha kwa furaha kuanzishwa kwa Tume ya Sayansi ya Ushirika wa Anglikana ili kuongoza na kuzingatia kazi yetu katika eneo hili, kutoa mawasiliano yenye ufanisi na rahisi kuhusu kazi inayotokana na Wito.

4.3 Tunatoa wito kwa shule zetu, seminari, vyuo vya kitheolojia na programu za mafunzo kukaribisha na kuingia katika mazungumzo ya kitheolojia na sayansi kama rasilimali waliyopewa na Mungu kwa ajili ya maisha ya imani na kuonyesha jinsi hekima ya imani inavyoweza kutolewa kwa kazi ya sayansi, ili watu wote wa Mungu, walei na waliosimikwa, waweze kuandaliwa vizuri ili wafanye vivyo hivyo kwa wale wanaowatumikia kama wanafunzi na watumishi wa umma. Tunaomba kwamba Tume mpya ya Elimu ya Kitheolojia katika Ushirika wa Anglikana iongoze katika hili.

4.4 Tunatoa wito kwa kila Kanisa la Ushirika limteue Askofu kiongozi wa Sayansi (ikiwa bado haijafanyika) na kuangalia uwezekano wa Tume ya wanasayansi na viongozi wa kanisa katika majimbo yao kupeleka mbele ajenda hii, kuunganishwa na kuungwa mkono na Mradi wa Sayansi wa Ushirika wa Anglikana.[vi] Tunaomba hasa kwamba wanasayansi vijana wakaribishwe kwenye tume hizi.

4.5 Tunatoa wito kwa kila mwanafunzi wa Kianglikana wakue katika uelewa wao wa sayansi kama sehemu muhimu ya ustawi wa wanafunzi wote na kwa utume wa kila kanisa, ili waweze kuchukua jukumu kubwa zaidi kama raia wa ulimwengu na kuwa Kanisa la Mungu kwa Dunia ya Mungu.

**5 Utekelezaji**

Mwitikio wa Wito huu utaongozwa na Tume ya Sayansi ya Ushirika wa Anglikana iliyozinduliwa katika Lambeth 2022 ikisaidiwa na timu ya wanasayansi na wanateolojia kutoka katika Ushirika wote. Kazi hiyo itawezeshwa na Mradi wa Sayansi wa Ushirika wa Anglikana, ambao utakuwa katika vyuo vikuu viwili au vitatu, kama vile Oxford, Cape Town na Chuo Kikuu cha St Paul, Limuru, Kenya.

Tume itatoa taarifa kwa vipindi vya kawaida kuhusu malengo na maendeleo yake.

Tume pia itaripoti katika mkutano ujao wa Lambeth Conference kuhusu maendeleo yaliyopatikana katika muongo huu muhimu.

## Melezo ya Mwisho

i. Angalia kwa mfano, Maazimio ya 1 na 2 ya Lambeth Conference ya mwaka 1978 na ufafanuzi wake ukurasa wa 65-67.

ii. ‘Kuwaandaa Viongozi wa Kanisa katika Zama za Sayansi’ (ECLAS) ilianzishwa mwaka 2013 ikilenga Uingereza na hatimaye Amerika ya Kaskazini ikiwa na malengo yaleyale **https://www.eclasproject.org**

iii. Askofu Mkuu wa Canterbury, Hotuba kwa Viongozi wa Imani, Februari 2021 **Askofu Mkuu wa Canterbury akihutubia viongozi wa imani wa kimataifa kabla ya mkutano wa COP26 wa mabadiliko ya hali ya hewa**

iv. Holy See: Imani na Sayansi, Wito kwa COP26 (Tamko la pamoja kutoka kwa viongozi 40 wa dini na wanasayansi wakubwa) **Holy See: Imani na Sayansi: Wito kwa COP26 - GOV.UK (www.gov.uk)**

v. Sayansi imekuwa na hatia katika historia ya ukoloni na hali hii bado inaonekana katika baadhi ya sehemu Ushirika. Ufa si tu kati ya ‘imani‘ na ‘sayansi’ bali ni suala tata zaidi.

vi. Maombi ya kufadhili mradi huu yamefanywa kwa wakfu mkubwa wa kimataifa.

# WITO WA LAMBETH
# HESHIMA YA BINADAMU

*Asifiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo! Ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili ili tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu... 1 Petro 1:3*

## 1 Azimio

1.1 Ndani ya karama nzuri ya Mungu ya uumbaji (Mwa. 1:31), Binadamu ameumbwa kwa mfano wa Mungu na kubarikiwa kwa uangalizi na upendo wa Mungu (Mwanzo 1.26-28). Hii inawapa wanadamu wote hadhi ambayo haiwezi kuchukuliwa. [i] "Wakati wowote tunapomtazama mwingine, tunaona upendo na utukufu wa Mungu usio na kikomo."[ii]

1.2 Ni katika utume wa Kristo ndipo tunajua neema ya Mungu na upendo mwaminifu wa Mungu kwa kila mwanadamu (Yn 3:16; Kol. 1:15–20; Rum. 5:18–19; 1 Kor. 15:22; 2 Kor. 5:14–17; I Kor. 2:9).[iii] Binadamu amepewa kuzaliwa upya katika tumaini hai kwa njia ya ufufuo wa Kristo (1 Pt.1:3; 2 Pt. 1:14). Kama wabeba sura ya Mungu, wanadamu wameitwa kumpenda Mungu na kupendana (1 Yoh. 4:11).[iv]

1.3 Uanuwai wa ajabu wa uumbaji wa Mungu unaonekana katika utofauti wa wanadamu. Kila mwanadamu "ni wa kipekee na ni siri ya kina ya thamani na hadhi isiyo na kifani".[v] Uanuwai huu miongoni mwa wanadamu na viumbe vyote ni mzuri na wa kupendeza. Pentekoste na maono ya Ufunuo 7:9 huonyesha jinsi uanuwai ulivyo zawadi nzuri kutoka kwa Mungu wakati, katika nguvu ya kuunganisha ya Roho Mtakatifu, inatumiwa katika huduma ya Mungu na kwa manufaa sisi kwa sisi.[vi]

1.4 Kristo tu ndiye sura kamilifu ya Mungu (Yoh. 10:30; Kol.1:15: 16 Wanadamu wote huuacha upendo wa Mungu na kuharibu sura ya Mungu.[vii] Tunakiri dhambi zetu na ushindi wa Mungu dhidi ya dhambi msalabani (1 Pt.2.24, 3:18; Rum. 5:8). Kuheshimu na kuhifadhi heshima ya kila mwanadamu kunajumuisha kuungama dhambi, toba, na msamaha. Ni katika Kristo, kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu, ndipo uwezo kamili wa mwanadamu huonekana.[viii] Ni karama ya kuzaliwa upya na kufanywa upya utambulisho ambao Kanisa, mwili wa Kristo, umeunganishwa kwa huo. Kama watu waliokombolewa na Kristo, Kanisa limeitwa kubeba sura ya Mungu, kuwa mwili wa Kristo duniani (1 Pt. 3.9-10; Wagalatia 3.28).

1.5 Kwa hiyo, umajumui wa kanisa hutangaza kwamba maisha ni matakatifu na watu wote wanastahili heshima na wanastahili mazingira ambamo wataishi maisha yao katika utumilifu wake.[xvii] Kutoka katika viwango hivyo vitakatifu hakuwezi kuwa na mpinzani mwaminifu.

## 2 Uthibitisho

Sisi ni watenda kazi pamoja na Mungu (1 Kor. 3:9) tulioitwa kulinda karama ya maisha ya binadamu na heshima ya binadamu wote.[x] Kama Yesu alivyoosha miguu ya yule aliyemkana na msaliti wake, tumeitwa kufuata mfano wake (Yn. 13:12–17, 34–35). Tumeitwa kupendana.

Matendo na mitazamo dhidi ya hadhi ya watoto wa Mungu ni dhambi. Kasumba za ukoloni, biashara ya utumwa kati ya bara la Amerika na Afrika, na matumizi mabaya ya madaraka yanaendelea kuathiri jamii zetu.[xi] Wengine wametajirika na wengine wamekuwa maskini. Mifumo ya kiuchumi ya kimataifa, iliyojengwa juu ya miundo isiyo ya haki ya unyonyaji, imeunda hali za kudhalilisha. Ukosefu mkubwa wa upatikanaji wa ardhi, afya na elimu, unyonyaji wa vijana, mazoea ya kazi yasiyo ya haki, unyanyasaji wa makabila madogo, wahamiaji na wakimbizi, unyama wa biashara haramu ya binadamu, mateso ya kidini, shinikizo kwa wale wanaoongozwa na uhuru wao wa dhamiri, ukandamizaji wa watu wa LGBTQ, unyanyasaji wa kijinsia, vita na unyanyasaji wa kingono katika migogoro, kwa sehemu, hudhihirisha dhambi kama hiyo. Ukarimu kwa wote na uaminifu kwa kila mmoja ni alama muhimu za jamii ya wacha Mungu (1 Pt. 4:8–10).

2.1 Mungu anakusudia kuwepo na jamii yenye utamaduni anuwai inayotoa uhai. Jitihada za kimishenari za mahali husika teolojia ya kimuktadha inathibitisha mapokezi ya kina, mabishano, kukubwaliwa, na kutumia Injili ya Yesu Kristo ndani na katika tamaduni zote.[xii] Hata hivyo, Uanglikana wa kimataifa mara nyingi ulijitokeza katika muktadha wa ukoloni. Tunatambua kuwepo athari inayoendelea ya Uanglikana wa kibeberu unaojihusisha katika vitendo vya kudhalilisha vinavyotokana na ukuu wa ubaguzi wa kitamaduni na rangi.[xiii] Kujizatiti kunakofanywa na Mkristo katika hadhi ya kibinadamu lazima afurahie uanuwai wa teolojia ya kimuktadha na kuzingatia shida ya Uanglikana katika ukoloni wa kikatili ulio dhahiri.

2.2 Mifumo ya kiuchumi isiyo ya haki inaharibu vibaya jamii maskini zaidi ulimwenguni.[iv] Maendeleo yalikuwa yamepatikana katika kupambana na umaskini.[xv] Hata hivyo, janga la kimataifa, kuongezeka kwa mfumuko wa bei, na vita vimeona kurudi nyuma kusikotarajiwa katika kupunguza umaskini. Dharura inayoendelea ya hali ya hewa (inayoonekana, kwa mfano, kuongezeka kwa joto kimataifa, kuongezeka kwa kina cha bahari, na hali ya tindikali kwenye bahari) inajenga zaidi kukosekana kwa utulivu na ukosefu wa chakula na kuhafifisha jitihada za kuondokana na umaskini na kujenga maendeleo endelevu sasa na baadaye.[xvi] Mwaka 2020, watu milioni 120-124 zaidi walirudishwa kwenye umaskini uliokithiri.[xvii] Mwaka 2022, inakadiriwa kuwa kati ya watu milioni 657 na milioni 676 wataishi katika umaskini uliokithiri.[xviii] Tunaombolezea takwimu hizi na namna ambavyo umasikini huathiri wanawake na wasichana kwa kiasi kikubwa.[xix] Kujizatiti kwa hadhi ya binaamu kunamaanisha kanisa linasimama katika mshikamano na maskini na waliotengwa na linashuhudia dhidi ya udhalimu kama maskini na waliotengwa.

4.3 Ubaguzi kwa misingi ya jinsia au mwelekeo wa kingono unatishia utu wa binadamu. Kutokana na uaminifu wa Kianglikana, na hasa uhuru wa majimbo, kuna kutokubaliana na wingi wa maoni juu ya uhusiano kati ya utu wa binadamu na mwelekeo wa kingono wa binadamu. Hata hivyo, tunapata uzoefu wa kulinda heshima katika kuimarisha mazungumzo. Ni ufahamu wa Ushirika wa Anglikana kwa ujumla kwamba “watu wote waliobatizwa, wanaoamini na waaminifu, bila kujali mwelekeo wa kingono ni viungo kamili vya Mwili wa Kristo” na wanapaswa kukaribishwa, kutunzwa, na kutendewa kwa heshima (I.10, 1998).[xx] Baada ya tafakari ya kina ya kiteolojia na mchakato wa utambuzi, majimbo mengi yanaendelea kuthibitisha kwamba ndoa ya jinsia moja hairuhusiwi. Azimio la Lambeth la I.10 (1998) lilisema kuwa “kuhalalisha au kubariki muunganiko wa watu wa jinsia moja” hauruhusiwi.[xxi] Majimbo mengine yamebariki na kukaribisha muunganiko/ndoa za watu wa jinsia moja baada ya tafakari ya kina ya kitheolojia na mchakato wa utambuzi. Kama Maaskofu tunaendelea kujizatiti kusikiliza na kutembea pamoja, licha ya sisi kutokubaliana sana kuhusu masuala haya.

## 3 Maombi Maalum (Miito)

Maandiko yanashuhudia utu wa asili na usawa wa wanadamu wote kwa sababu wote wameumbwa kwa mfano wa Mungu. Katika utofauti mkubwa wa kikabila na kitamaduni wa Usharika wa Anglikana wote wameumbwa kwa mfano wa Mungu. Wote ni sawa. Hakika, ni nia ya Mungu kupangilia utajiri wa tamaduni za ulimwengu katika ufunuo wa mwisho na mkamilifu wa ukombozi wa utukufu wa Mungu (Ufu. 21:24). Kwa hiyo, maaskofu waliokusanyika katika mkutano Lambeth 2022 huto wito kwa Kanisa kulinda heshima ya viumbe wote, tamaduni, na binadamu. Tunatoa wito Kwa Ushirika:

3.1 Kuunga mkono uanzishwaji wa Tume ya Askofu Mkuu ya Hatua za Ukombozi (ACRA).

Kazi hii itakuwa na, angalau, mikazo minne. Kwanza, Askofu Mkuu wa Canterbury anapaswa kuitisha ACRA kama kikundi cha wanatheolojia katika Ushirika, chini ya uenyekiti wa Mwanateolojia Mkuu wa Dunia (tunapendekeza awe kiongozi kutoka jamii ambayo ilipata ukoloni na utumwa). ACRA itapitia ripoti na maelezo ya uchunguzi unaozalishwa na Makamishna wa Kanisa la Uingereza katika uhusiano wa kihistoria wa kanisa katika utumwa wa uliohusisha bara la Afrika na Marekani.[xxii]

Pili, ACRA itaanzisha na kuchapisha teolojia kamilifu za hatua za ukombozi na ulipaji fidia, zilizojikita katika mapokeo makuu ya maandiko ya ukombozi wa Mungu katika Kristo, na wito wa kanisa kwa huduma ya upatanisho (2 Kor. 5:17-19.[xxiii] Tunamwomba Askofu Mkuu wa Canterbury (kama Mwenyekiti wa Bodi ya Watawala ya Makamishina wa Kanisa) ili kuhakikisha kwamba theolojia hii inaunda mwitikio wa Makamishina wa Kanisa kuhusu uhusiano wa kanisa na ukoloni na utumwa.

Tatu, ACRA, kwa kushauriana na kazi ya Makamishna wa Kanisa, itatambua vigezo, jamii, na programu ambazo zitatumika kama ushuhuda mpana wa Ushirika katika hatua ya ukombozi.

ACRA itatoa ripoti za maendeleo ya kila robo mwaka kwa Askofu Mkuu wa Canterbury na Kamati ya Kudumu ya Baraza la Ushauri la Anglikana.

3.2 Hatua za shughuli zinazofadhiliwa za ulinzi wa jamii katika Ushirika wa Anglikana

Hatua kama hiyo itamaanisha, inapowezekana, kushawishi serikali kwa ajili ya hatua za ulinzi wa jamii. Pia itamaanisha Ushirika wa Anglikana unatekeleza ulinzi wa jamii.

Kwanza, kwa kushauriana na vyanzo husika na wataalamu, katika mkutano ujao wa Maaskofu Wakuu, Maaskofu Wakuu wanapaswa kuchunguza pamoja maana na athari za ulinzi wa jamii katika mazingira yao.[xxiv] Maaskofu Wakuu wataongoza katika kushuhudia uwezekano wa kubadilisha maisha ya miradi ya ulinzi wa jamii wakati wakiwaandaa maaskofu wao na dayosisi kufanya vivyo hivyo katika mazingira ya eneo husika.

Pili, kwa sababu umaskini ni “shida ya aina nyingi ambayo inahitaji njia nyingi na jumuishi”, nyenzo ambazo ni za kiuchumi, kisiasa, kijamii, mazingira, taasisi, na kiroho zinapaswa kuhamasishwa.[xxv] Katika jitihada za kuimarisha njia za kiroho na za kufikiria za kutokomeza umaskini, haswa umaskini wa vijana, tunatoa wito kwa ACC kuanzisha Mfuko wa Ubunifu wa Anglikana (AIF). Mfuko huu utatoa msaada wa kifedha kwa vijana (miaka 18-30) ambao wanaanzisha miradi au biashara zinazopambana na umaskini kwa kuzingatia zaidi ulinzi wa jamii. Kwa kurejelea kipengele cha 3.1, mpango huu unaweza kupata ufadhili unaoendelea kama utekelezaji wa ACRA na majibu ya Makamishna wa Kanisa kuhusu udhalimu wa kihistoria wa utumwa.

3.3 Kupanua kazi ya Ofisi ya Ushirika wa Anglikana ili Kuhimiza Heshima ya Binadamu kwa kuzingatia Mwelekeo wa Kingono na Jinsia .

Tunatoa wito kwa ACC (kulingana na mitandao husika na idara ya ACO na taarifa na Lambeth 1998 azimio la I.10), kuchunguza kama kazi yake juu ya Haki ya Jinsia inapaswa kupanuliwa ili kukuza maono na desturi za majimbo kuelekea utu wa binadamu kwa kuzingatia si tu jinsia lakini pia mwelekeo wa kingono. Katika ACC-19 ripoti za majimbo na baina ya majimbo kuhusu suala hili zinapaswa kupokelewa na mapendekezo zaidi kutolewa.

## Melezo ya Mwisho

i. Tume ya Kudumu ya Jumuiya yote ya Anglikana juu ya Umoja, Imani na Utaratibu (IASCUFO), Tumeumbwa kwa Sura ya Mungu: Karama ya Mungu na Wito kwa Binadamu: Anthropolojia ya Anglikana: Umoja, Imani na Utaratibu Makala ya 3 (London: ACC, 2021), 9, 12, 14-25, 42 **https://www.anglicancommunion.org/media/460188/UFO_IASCUFO_Papers-3-and-4 – God-So-Loved-the-World_v2_en.pdf** Angalia pia matoleo ya Brian Brock na John Swinton. Ulemavu katika Utamaduni wa Kikristo: Msomaji (Grand Rapids: Eerdmans, 2012); Baraza la Makanisa la Ulimwengu, *Kipawa cha Kuwa: Kuitwa kuwa Kanisa la Wote na kwa Wote* (2016) **https://tinyurl.com/7kyvdnrb**

ii. IASCUFO, *Tumeumbwa kwa Sura ya Mungu*, 24

iii. Tume ya Kimataifa ya Majadiliano ya Kitheolojia ya Anglikana-Othodoksi (ICAOTD), Katika Sura na Mfano wa Mungu: Anthropolojia Iliyojaa Tumaini ("Taarifa ya Buffalo", 2015), 5-12. Lambeth 1998, I.10c; IASCUFO, Tumeumbwa kwa Sura ya Mungu, 75-77.

iv. IASCUFO, *Tumeumbwa kwa Sura ya Mungu*, 34–40.

v. IASCUFO, *Tumeumbwa kwa Sura ya Mungu*, 24.

vi. IASCUFO, *Tumeumbwa kwa Sura ya Mungu*, 10–11.

vii. IASCUFO, *Tumeumbwa kwa Sura ya Mungu*, 12, 50–57.

viii. IASCUFO, *Tumeumbwa kwa Sura ya Mungu*, 9–11, 30–35.

ix. ICAOTD, Katika Sura na mfano wa Mungu; Lambeth 2008, Sehemu C (Haki za Binadamu na Jamii); Lambeth 1998, I.1, 2, 4, 5, 9, 14, 15; III.21, 22.

x. IASCUFO, *Tumeumbwa kwa Sura ya Mungu*, 26–30.

xi. IASCUFO, Tumeumbwa kwa Sura ya Mungu, 53-54. Angalia Jeremy M. Bergen, *Toba ya Kikanisa*: *Makanisa Yanakabiliana na Dhambi Zao za Zamani* (London: T&T Clark, 2011); Shirika la Kazi Duniani (ILO), Tembea ukiwa Huru, na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM), *Makadirio ya Kimataifa kuhusu Kazi ya Kilazimishwa ya Utumwa wa Kisasa na Ndoa ya Kulazimishwa* (Geneva: Machapisho ya ILO, 2022)

xii. Angalia Lamin Sanneh, *Kutafsiri Ujumbe: Athari ya Umishonari kwa Utamaduni toleo lililorejewa*. (Maryknoll: Orbis, 2009); Jehu H. Hanciles, *Uhamiaji na Utengenezaji wa Ukristo wa Ulimwengu* (Grand Rapids: Eerdmans, 2021); William L. Sachs na Robert S. Heaney, *Ahadi ya Anglikana* (London: SCM, 2019).

xiii. Angalia Rowan Strong, Uanglikana na Dola ya Uingereza (Oxford: Oxford University Press, 2007; Ian T. Douglas na Pui-lan Kwok, *Zaidi ya Uanglikana wa Kikoloni: Ushirika wa Anglikana katika Karne ya Ishirini na Moja* (New York: Church Publishing, 2000).

xiv. Angalia IASCUFO, *Tumeumbwa kwa Sura ya Mungu*, 52-54.

xv. Andrea Peer na Sevil Omer, "Umaskini wa ulimwengu: Ukweli, Maswali yaulizwayo sana, na jinsi ya kusaidia" **https://www.worldvision.org/sponsorship-news-stories/global-poverty-facts**, Agosti 23, 2021 (ilipatikana Juni 10, 2022).

xvi. Umoja wa Mataifa, Mkutano Mkuu, Kikao cha 73 (18 Oktoba, 2018), Kamati ya Pili, Ajenda ya 24 (a), "Kuondoa umasikini na masuala mengine ya maendeleo: utekelezaji wa Muongo wa Tatu wa Umoja wa Mataifa wa Kuondoa Umaskini (2018-2027), 4. IASCUFO, Tumeumbwa kwa Sura ya Mungu, 12-13, 58-67.

xvii. **https://sdgs.un.org/goals/goal1** ilipatikana Juni 10, 2022.

xviii. "Umaskini uliokithiri" hupimwa kuwa watu wanaoishi chini ya dola 1.90 kwa siku. Tazama Daniel Gerszon Mahler, Nishant Yonzan, Ruth Hill, Christoph Lakner, Haoyu Wu na Nobuo Yoshida, "Janga, bei, na umaskini" **https://blogs.worldbank.org/opendata/pandemic-prices-and-poverty**, Aprili 13, 2022 (ilipatikana Agosti 10, 2022). Angalia **https://www.un.org/en/global-issues/ending-poverty** Ilipatikana June 11, 2022. Kwa taarifa juu ya mabadiliko ya hali ya hewa na mifumo ya uhamiaji angalia Jopo la Serikali juu ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa, Mchango wa Kikundi cha Kufanya Kazi cha III kwa Ripoti ya Tathmini ya Sita ya Jopo la Serikali juu ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa, "Mabadiliko ya Hali ya Hewa 2022: Uhamiaji wa Mabadiliko ya Hali ya Hewa" (Aprili 2022), 2-54 - 2-55; 3-96 - 3-109. **https://www.ipcc.ch/report/ar6/wg3/ IPCC_AR6_WGIII_FinalDraft_FullReport.pdf** ilipatikana Juni 27, 2022.

xix. Umoja wa Mataifa, Mkutano Mkuu, Kikao cha 73 (18 Oktoba, 2018), Kamati ya Pili, Ajenda ya 24 (a), "Kuondoa umasikini na masuala mengine ya maendeleo: utekelezaji wa Muongo wa Tatu wa Umoja wa Mataifa wa Kuondoa Umaskini (2018-2027), 3.

xx. Bora 1998, 1.10 c, d

xxi. Hanse 588 “Jasmine”

xxii. **https://www.churchofengland.org/sites/default/files/2022-06/Church%20 Commissioners%20 research%20report%20final.pdf** ilipatikana Juni 28, 2022

xxiii. IASCUFO, Tumeumbwa kwa Sura ya Mungu, 75-77. Angalia IASCUFO, Ukuu wa Mungu na Wokovu Wetu: Taarifa ya Kitheolojia ya Anglikana: Umoja, Imani na Utaratibu Makala ya 4 (London: ACC, 2021), 82-84.

xxiv. Ulinzi wa jamii ni mpango au mfumo wowote uliowekwa ili kuwalinda wafanyakazi dhidi ya mabadiliko makubwa au ya kutisha katika hali za kazi. Ulinzi wa jamii unamaanisha waajiri kushiriki hatari na wafanyakazi wao. Ulinzi kama huo unaweza kuwa katika mfumo wa, kwa mfano, mafao ya pensheni, upatikanaji wa mikopo ya kiwango cha chini, na upatikanaji wa huduma za afya za ruzuku au za bila malipo. Kwa maelezo zaidi kuhusu dhana ya “kugawana hatari” angalia Truman Packard, Ugo Gentilini, Margaret Grosh, Philip O’Keefe, Robert Palacios, David Robalino, na Indhira Santos, *Protecting All: Risk Sharing for a Diverse and Diversifying World of Work* (Washington DC: Benki ya Kimataifa ya Ujenzi na Maendeleo/Benki ya Dunia, 2019) **https://bitly.ws/zBmR** Juni 21, 2022.

xxv. Umoja wa Mataifa, Mkutano Mkuu, Kikao cha 73 (18 Oktoba, 2018), Kamati ya Pili, Ajenda ya 24 (a), “Kuondoa umasikini na masuala mengine ya maendeleo: utekelezaji wa Muongo wa Tatu wa Umoja wa Mataifa wa Kuondoa Umaskini (2018-2027)”, 3.

# WITO WA LAMBETH
# UMOJA WA KIKRISTO

*Neno la mwisho ni hili; muwe na nia moja, wenye kuhurumiana, wenye kupendana kama ndugu, wasikitikivu, wanyenyekevu. 1 Petro 3: 8*

## 1 Azimio

*Hadithi yetu ya Kiekumeni*

1.1 Zaidi ya miaka mia moja iliyopita, maaskofu wa Ushirika wa Anglikana, waliokusanyika katika Lambeth Conference ya mwaka 1920, walitoa Wito kwa Wakristo wote. Ndani yake, walizungumza kuhusu shauku yao kubwa ya kutafuta umoja wa Wakristo wote katika Kanisa linaloonekana kuwa na umoja, ambalo lingeshuhudia nguvu ya kupatanisha ya Injili, na kuwaita mataifa yote kufanya toba na kuwa kwenye imani. Kukutana pamoja kama maaskofu katika Lambeth Conference mwaka 2022 tunasikia wito wao ukisikika upya na sasa tuweze kujizatiti kujitahidi kwa ajili ya umoja wa Kanisa.

1.2 Wito kwa Wakristo Wote uliwakilisha hatua kubwa iliyofanywa kuelekea katika ushiriki wa Anglikana katika harakati ya kiekumeni ulimwenguni kote ambayo ilikuwa imeanza mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Tangu wakati huo, harakati hii imepiga hatua kubwa, na uhusiano kati ya tamaduni tofauti za Kikristo umebadilishwa. Si wageni tena, uwezekano wa kuwa maadui, kwa kila mmoja, kumekuwa na juhudi kubwa za kuimarisha koinonia na utume. Waanglikana wameshiriki katika muungano wa Makanisa kadhaa katika Asia ya Kusini, na jitihada zote za kimataifa na za kikanda za ushirika kamili. Tunaendelea kufurahia Mkataba wa Bonn na Umoja wa Utrecht, na uhusiano mwingi mzuri wa ushirika, kwa mfano na baadhi ya Makanisa ya Kilutheri. Pia kuna makubaliano mengine ya kujizatiti na mazungumzo, ikiwa ni pamoja na ushiriki katika vyombo mbalimbali kama vile Baraza la Makanisa Duniani.

1.3 Uekumeni leo unachukua sura nyingi. Ambapo Makanisa yamefanya kazi pamoja katika masuala ya amani na haki, maisha yetu ya kawaida na ushuhuda umeimarishwa sana. Makanisa yamezidi kuzungumza na kufanya kazi pamoja kuhusu mazingira na utunzaji wa uumbaji. Tunakaribisha ukuaji wa uekumene wa kiroho, na desturi ya Wakristo kusali pamoja, wakati mwingine katika mazingira ya jumuiya za kiekumeni za kukusudia kama vile Jumuiya ya Mtakatifu Anselm, iliyo katika Lambeth Palace.

*Changamoto Zinazoendelea*

1.4 Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni maendeleo katika kufanikisha umoja katika masuala ya imani na utaratibu yamepungua. Licha ya muunganiko mkubwa katika masuala ya mafundisho, makubaliano juu ya mifumo ya utawala imeonekana kuwa migumu zaidi na mifumo tofauti ya utawala na mapokeo ya kanisa katika Makanisa si rahisi kupatanishwa. Katika ngazi ya eneo husika Kanuni ya Lund (kwamba Makanisa yanapaswa kutafuta kufanya kazi pamoja isipokuwa pale ambapo ‘tofauti kubwa za kusadikisha zinawalazimisha kutenda tofauti’) kwa ujumla inakubaliwa, lakini inaweza kuwa vigumu kutekelezwa.

1.5 Kutofautiana kwa Kanisa ni jeraha linaloendelea na lenye uharibifu katika mwili wa Kristo. Tunasikitika kwamba mgawanyiko kati ya waliobatizwa husababisha utengano: ukosefu wa utambuzi wa pamoja wa sakramenti na huduma zetu na huzuni ya kudumu ya kutoweza kwetu kushiriki Ushirika Mtakatifu pamoja. Mgawanyiko kama huo hudhoofisha ushuhuda wa Kanisa kwa Injili ya upatanisho wakati ambapo, katika sehemu nyingi za dunia, kanuni za serikali, mateso na hata ugaidi huwafanya Wakristo kuwa katika mazingira magumu katika maisha na ushuhuda wao.

## 2 Uthibitisho

*Ahadi yetu ya Anglikana*

2.1 Kwa kuanza na Imani za Msingi za Chicago-Lambeth (1886/1888), kumekuwa na ufafanuzi mwingi wa lengo la umoja tunaoutafuta. Baraza la Ushauri la Anglikana (ACC-14, 2009) lilikubali Kanuni Nne zifuatazo za Uekumene:

- Lengo: Umoja kamili halisi wa Kanisa;
- Kazi: kutambua na kulipokea Kanisa ndani ya kila mmoja;
- Mchakato: umoja kwa hatua;
- Maudhui: imani ya pamoja, sakramenti na huduma.

2.2 Sisi, maaskofu wa Ushirika wa Anglikana, sasa tunathibitisha kujizatiti kwetu kutafuta umoja wa mwili wa Kristo, ambao ni Kanisa. Katika somo letu la Waraka wa Kwanza wa Petro, tumekumbushwa kwamba Kanisa ni uumbaji wa Mungu, uliowekwa juu ya jiwe moja la msingi, ambalo ni Yesu Kristo. Katika wito wa Mungu, Kanisa ni moja la 'wateule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, milki ya pekee ya Mungu', walioitwa 'kutangaza sifa za Yeye aliyetuita kutoka gizani kuingia katika nuru yake ya ajabu' (1 Petro 2.9).

2.3 Kwa hivyo tunathibitisha:

2.3.1 Kwamba Makanisa ya Ushirika wa Anglikana ni sehemu ya Kanisa moja, takatifu, la kimajumui na la kitume;

2.3.2 Kwamba wito wa Ushirika wa Anglikana ni pamoja na kujizatiti kutafuta umoja unaoonekana wa Kanisa la Kristo;

2.3.3 Kwamba, licha ya mgawanyiko wetu, tunatambua katika Makanisa mengine ya Kikristo matunda ya kazi ya Roho Mtakatifu, kujizatiti katika kutangaza Injili na uaminifu kwa taasisi ya Yesu ya Sakramenti ambazo tunathamini katika maisha yetu wenyewe;

2.3.4 Kwamba katika kila ngazi ya maisha ya kanisa Makanisa ya Anglikana yanaweza kujifunza kutoka kwa Makanisa mengine, ushirika na mapokea na kujifunza, kupokea karama za neema;

2.3.5 Kuwa Waanglikana wanapaswa kufanya kazi pamoja katika utume na huduma na Makanisa mengine pale inapowezekana, kuelekea katika umoja kamili hai ambao tunaamini ni mapenzi ya Mungu na wito wetu.

## 3 Maombi Maalum (Miito)

3.1 Wito wa kuchukua hatua

Tunatoa wito kwa Vyombo vya Ushirika, Makanisa na washiriki wa Ushirika wa Anglikana:

3.1.1 Kufanya upya kujizatiti kwao katika utafutaji wa haraka wa umoja kamili wa Kanisa ulio hai;

3.1.2 Kupokea na kuendeleza matunda ya mahusiano yetu ya kiekumene;

3.1.3 Kujenga uhusiano wa karibu na Makanisa mengine katika Majimbo yao;

3.1.4 Kutafuta maridhiano na umoja hata ndani ya familia ya Makanisa ya Anglikana, kwa kutambua kwamba kutoelewana ndani ya Ushirika wa Anglikana kumesababisha kuundwa kwa makanisa na makundi yaliyojitenga ambayo, ingawa bado yanatumia mapokeo ya Anglikana, tumegawanyika.

3.1.5 Kufanya kazi na ndugu na dada zetu katika Makanisa mengine katika utume wa kutangaza habari njema ya Kristo na kushughulikia mahitaji ya ulimwengu;

3.1.6 Kupaza sauti kwa niaba ya ndugu na dada wanaoteswa: maana kiungo kimoja cha mwili kinapoumia mwili wote unaumiwa pamoja nacho;

3.1.7 Kuona yaliyo mema zaidi kwa wengine na kutafuta kile tunachoweza kupokea kutoka katika utajiri wa desturi ambazo si zetu;

3.1.8 Kutafuta fursa za mazungumzano ili kuondokana na zile tofauti za kiteolojia na kikanisa zinazobaki kama vikwazo vya ushirika kamili unaoonekana wa Kanisa la Kristo katika ngazi za mahali husika, kanda na za kimataifa, kuanzisha mahusiano rasmi ya ushirika na Makanisa mengine pale inapowezekana na kufanya kazi kwa lengo la umoja kamili ulio hai.

3.2 Mwaliko wa Kiekumeni

Hati ya Imani na Utaratibu ya Baraza la Makanisa Ulimwenguni, Kanisa: Kuelekea Kuwa na Maono ya Pamoja inaelezea kazi ya kiekumeni kama wito kwa Makanisa kuelekea kupata 'umoja katika imani, umoja katika maisha ya sakramenti, na umoja katika huduma' (aya 67). Katika nia hii, tunawaalika washirika wetu wa kiekumene:

3.2.1 Kutusaidia katika kuelewa kina na utofauti wa maisha katika Kristo, na kile tunachoweza kujifunza kutoka kwa kila mmoja;

3.2.2 Kuyaalika Makanisa ya Anglikana ambayo ni jirani wao washiriki pamoja nao katika mipango ya mahali husika kutangaza injili, kuhuisha uhai wa Kanisa na kutumikia jamii kwa manufaa ya wote;

3.2.3 Kufanya kazi nasi katika kushiriki utajiri wa urithi wetu wa imani, na karama zile tofauti ambazo Mungu ametupa katika historia na uzoefu wetu uliotenganishwa (rej. 1 Petro 4. 10);

3.2.4 Kujiunga nasi katika kufuata hatua zinazoongoza kupata umoja kamili halisi.

3.2.5 Katika kushukuru kupata mafanikio ya harakati za kiekumene, tunahimizana kuchukulia kwa uzito juhudi za kiekumene katika maisha na huduma zetu, tukikumbuka wakati wote sala ya Bwana wetu mwenyewe kwamba wote wawe na umoja (Yohana 17. 20).

**4 Utekelezaji**

4.1 Jukumu la kuhamasisha na kufuatilia utekelezaji wa wito huu ndani ya Makanisa wanachama na Vyombo vya Ushirika ni la Baraza la Ushauri la Anglikana, likifanya kazi kupitia Tume ya Kudumu ya Makanisa ya Anglikana kuhusu Umoja, Imani na Utaratibu (IASCUFO) na Ofisi ya Ushirika wa Anglikana;

4.2 Tunatoa wito kwa ACC na Katibu Mkuu kuhakikisha kuwa rasilimali za kutosha zinapatikana ili kuwezesha kazi hii;

4.3 Tunawaalika IASCUFO kufuatilia na kusimamia maendeleo na kuripoti mara kwa mara kwenye ACC;

4.4 Tunayaalika makanisa Wanachama kuripoti mara kwa mara kwenye IASCUFO, kupitia Idara ya ACO ya Umoja, Imani na Utaratibu, kuhusu maendeleo na changamoto katika eneo hili.

# WITO WA LAMBETH
# UTUME NA UINJILISTI

## 1 Utangulizi

1.1 Tukiwa wale walioitwa kumtumikia Kristo katika huduma ya kiaskofu katika makanisa ya Anglikana, tunafurahi kutangaza wito huu kwa ajili ya Uinjilisti.

1.2 Watu wa Mungu wamechaguliwa, wamewekwa wakfu, wameandaliwa, na kutumwa katika dunia ya Mungu 'ili mweze kutangaza sifa zake yeye aliyewaita ninyi kutoka gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu' (1 Petro 2: 9). Kwa maana sisi ambao ni wapokeaji wa huruma kuu ya Mungu katika Kristo, sisi ambao tumepewa 'kuzaliwa upya katika tumaini lililo hai kwa njia ya ufufuo wa Yesu Kristo kutoka kwa wafu', sisi ambao tuna 'urithi ambao hauwezi kuharibika au kupotea', tumejazwa na Roho Mtakatifu 'aliyetumwa kutoka mbinguni' ambaye hutugeuza kutoka kuwa tunajihudumia wenyewe kutangaza injili nzuri, ambayo malaika wametamani kuwaangalia wote. Umoja wetu wa roho, maisha yetu katika kuitikia neema ambayo ni yetu, mateso yetu, kiujizatiti kwetu, huduma, ukarimu na matumaini yanaonekana katika maisha ili wote waweze kumtukuza Mungu anayekuja kama hakimu wa watu wote.

## 2 Azimio

2.1 Kila Kanisa kote katika Ushirika wa Anglikana kwa furaha na ujasiri hushiriki wito huu wa kutangaza habari njema za wokovu wa Mungu wa ulimwengu katika Kristo Yesu. Alama yetu ya kwanza ya Utume inatuagiza: Kutangaza Habari Njema ya Ufalme.

2.2 Uinjilisti ni tangazo la injili ya yule aliyekuwa amekufa lakini sasa yuko hai, Kristo Yesu na Ufalme wa Mungu anaouanzisha. Akiwezeshwa na Roho Mtakatifu kila Mkristo ni shahidi wa Yesu Kristo.

*Msiogope kutisha kwao, wala msifadhaike; bali mtakaseni Kristo Bwana mioyoni mwenu. Muwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa heshima. [1 Petro 3: 14-16]*

2.3 Utume wetu wote na uinjilisti huanza na utume wa Mungu; Mungu anachagua kuwa kwa ajili yetu katika kujenga na upendo uokoao kuwa kwa ajili yetu. Kristo Yesu ni mwinjilisti mkuu ambaye, kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, anafanya kazi daima, kwa uaminifu na kwa bidii ili kuwavuta watu wote kwake. Papa Francis asema, 'ni kazi ya Mungu ya kwanza kabisa'. Akiwezeshwa na Roho Mtakatifu, anawaita watu wake wafanye kazi pamoja naye, kama mawakala wake wa habari njema.

2.4 Kila kanisa katika Ushirika wetu lina asili yake katika utume wa Mungu. Mwaka 597 St Augustine alifika Canterbury, alipotumwa na Papa Gregori Mkuu, kutangaza habari njema. Ushirika wetu ni ushahidi wa wito na nguvu ya habari njema ya Kristo katika kila nchi na utamaduni. Kila kanisa lilianzishwa kwanza kwa sababu Mungu alimtuma mtu kutangaza habari njema ya Kristo na, kupitia uwezo wa Roho Mtakatifu, kanisa liliundwa kama matokeo yake.

2.5 Kama wale tulioitwa kuongoza, sisi ni wale waliopewa jukumu la kuongoza utume wa kanisa; sisi ni ishara ya kitume ya utume wa Kristo wa kuhubiri Injili kwa ulimwengu wote, na kufanya watu wote wa kila taifa kuwa wanafunzi.

## 3 Uthibitisho

Kwa kusukumwa na upendo wa Kristo, ambao umemwagwa ndani ya mioyo yetu na Roho Mtakatifu, tunasadikishwa na hitaji la ulimwengu la kupokea wokovu na ukombozi ambao injili inatangaza - kwamba wote ambao Mungu amewafanya wasikie habari njema, kwa njia ambayo wanaweza kuitikia kwa imani kwa yote ambayo Mungu amefanya katika Kristo. Habari njema ya neema na rehema, ya toba na msamaha, ya upatanisho na uwakili, ya matumaini na ya milele ni ujumbe ambao ulimwengu unakufa bila kusikia. Lakini injili ni kwa ajili ya ulimwengu huu ulioanguka. Mungu anawapenda wanadamu. Mungu anaupenda ulimwengu. "Si mwanadamu wa kufikirika, bali wanadamu kama walivyo; si ulimwengu wa kufikirika, bali ulimwengu halisi. Mungu anamwita kila mtu kupitia upendo wake mkuu, kwa hivyo ni muhimu kwamba wale ambao hawajawahi kusikia habari hii njema waweze kuisikia kwa njia wanayoielewa, ili waweze kuiitikia. Roho Mtakatifu amemiminwa ndani ya mioyo yetu ili tuweze kuishi kama mashahidi waaminifu wa Yesu Kristo.

## 4 Maombi Maalum (Miito)

4.1 Kila jimbo na kila kanisa litafute kwa bidii kufanywa upya kwa ajabu na nguvu ya habari njema ya Kristo.

4.2 Kila jimbo na kila kanisa lijizatiti kwenye maombi, kusikiliza na kutambua, kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, ili tuweze kuishi kuwa mashuhuda waaminifu wa Kristo na kutangaza Injili katika uhalisia. Hii ni pamoja na kuomba Roho Mtakatifu afanye kazi ndani ya mioyo na akili ili ujumbe wa injili uweze kupokelewa na kuzaa matunda.

4.3 Kwa kutii agizo la Kristo mwenyewe, kila kanisa lijizatiti kufanya matendo ambayo kwa makusudi yanaleta habari njema ya Kristo, ili wote waweze kuusikia wito wa Kristo na kumfuata.

4.4 Kila Mkristo apokee kwa furaha wito wa kuwa shahidi wa Yesu Kristo, akiomba kwamba kwa njia hii angalau mtu mwingine mmoja kila mwaka aweze kupokea imani na kukua kama mwanafunzi.

4.5 Kwamba sisi kama Ushirika wa Anglikana tuombeane katika huduma hii na kujizatiti kusikiliza, kujifunza na kupata faraja pamoja katika Wito huu.

4.6 Ili maaskofu waandaliwe na kuwezeshwa kuongoza katika uinjilisti huu. Kwa kufuata mfano wa kitume, sisi maaskofu tunapaswa kuwaongoza watu wa Mungu katika dunia ya Mungu kwa kutangaza kwa ujasiri.

4.7 Kwa kila dayosisi kuthamini, kufundisha, kutuma na kupokea wainjilisti.

4.8 Kwa kila dayosisi kujizatiti upya na kiububifu ili kuyahuisha makanisa na kuanzisha makanisa mapya kwa njia zinazofaa mazingira husika, ili kuwafikia wale ambao bado hawajapata kusikia Injili.

4.9 Kwa makanisa yanayoteswa yasaidiwe katika ushuhuda wao, ili walindwe na kusimama imara katika imani yao.

4.10 Tunatoa wito kwa Katibu Mkuu kusaidia na kufuatilia maendeleo katika maeneo haya kwa msaada wa Tume ya Uinjilisti na Uanafunzi, na kurudisha kuripoti kwenye ACC inayofuata.

# WITO WA LAMBETH
# UHUSIANO BAINA YA IMANI

**1 Utangulizi**

1.1 Katika ulimwengu wa tofauti za kidini, kama muktadha wa wale wanafunzi wa Kikristo ambao barua ya kwanza ya Petro ilielekezwa kwao, kanisa ni shahidi wa tumaini la habari njema ya wokovu katika Yesu Kristo (1 Petro 3:15-16), ishara ya baraka na huduma kwa jamii pana (1 Petro 2: 12), na matarajio ya utukufu wa Mungu katika Kristo ambayo yatafunuliwa kwa wote kwa uaminifu wake katikati ya uadui na mateso (1 Petro 4: 13-14).

**2 Azimio**

2.1 Yesu Kristo alipopaa kwenda mbinguni, aliahidi karama ya Roho Mtakatifu kwa wanafunzi wake ili waweze kuwezeshwa na maisha yake mpya ya ufufuo ili wawe mashahidi wake “hata miisho ya dunia” (Matendo 1:8).

2.2 Changamoto inayoendelea kwa Waanglikana ni jinsi tunavyopaswa kuwa Kanisa la Mungu kwa Dunia ya Mungu tunapoishi na watu wa imani tofauti. Kwa wengine katika Ushirika wa Anglikana kuna uhuru wa kuwaita watu katika ubatizo na uanafunzi, na majirani zetu wa tamaduni zingine za kidini wanaweza pia kuwa washirika katika kazi kwa faida ya wote, kukabiliana na maeneo ya pamoja yenye shida kama vile janga au mabadiliko ya hali ya hewa. Katika mazingira mengine, hata hivyo, Waanglikana wanakabiliwa na uadui na hata mateso. Hii ndiyo sababu Mtandao wa Masuala Baina ya Imani wa Ushirika wa Anglikana (“NIFCON”) ulianzishwa mnamo mwaka 1993 kwa mamlaka ya Lambeth Conference ya 1988 ili kushiriki hadithi za kukutana na waumini wengine katika sehemu tofauti za Ushirika.

2.3 Katika Lambeth Conference ya mwaka wa 2008, Upendo wa Ukarimu: ukweli wa injili na wito kwa ajili ya mazungumzo, uliwasilishwa na kupokelewa.[i] Katika roho ya Katiba Muhimu ya Kichungaji ya Romani Katoliki ya Vatican II, Nostra Aetate, Lambeth Conference alikiri kwamba “Kama washiriki wa Kanisa la Mungu wa Utatu, tunapaswa kukaa kati ya majirani zetu wa imani tofauti kama ishara ya uwepo wa Mungu kwao, na tunatumwa kushirikiana na majirani zetu kama mawakala wa utume wa Mungu kwao”. Upendo wa Ukarimu ulitambua utofauti wa mazingira kwa mifumo hii yote ya kuhusika na kushiriki katika Ushirika wa Anglikana, “iwe kama jamii ya watu wachache au ya watu wengi, iwe katika maeneo ya hatari au usalama, iwe katika uhusiano wa mazungumzo au mvutano”.[ii]

2.4 Licha ya muktadha wetu, majirani zetu wa tamaduni zingine za kidini wote wameumbwa kwa mfano wa Mungu, na kama Wakristo tunaitwa kuwapenda wengine kama tunavyojipenda sisi wenyewe.

**3 Uthibitisho**

3.1 Sisi Maaskofu wa Ushirika wa Anglikana, tuliokusanyika katika Lambeth Conference mwaka 2022, kwa hivyo tunathibitisha kujizatiti kwetu kumshuhudia Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi kupitia huduma ya uaminifu, inayofanana na Kristo na kwa kutangaza kwa unyenyekevu habari hii njema kati ya watu wa dini na imani tofauti.

3.2 Kukita mizizi kwa Kanisa na kuwa na deni kutokana na hadithi za Kiyahudi kunamaanisha kuwa kuna mfungamano wa muundo na msingi wa imani nyingine katika kukutana kwake na Uyahudi, *ulio dhahiri zaidi katika Maandiko hayo yanayotumiwa pamoja*. Tunakubali kwamba historia ya aibu ya mahusiano ya Kikristo na Kiyahudi inalipa kanisa jukumu fulani la kukataa na kushinda hali ya kupinga Uyahudi katika teolojia yake, liturujia na mahubiri.

3.3 Tunatambua kwamba kujizatiti kwetu katika 'Alama Tano za Utume' kunamaanisha uhusiano na watu wa mapokeo mengine ya kidini ndani ya utume wa Mungu katika Kristo, unaoeleweka kwa ujumla, na kila muktadha na uhusiano utaamua jinsi 'Alama hizi za Utume' zinavyowekwa pamoja.

3.4 Katika dunia ambapo kuna ongezeko la changamoto ambazo kuathiri jamii zetu zote, jinsi tunavyofanya kazi na damaduni nyingine za kidini kwa manufaa ya wote ni ushahidi wa ushiriki wetu katika kazi ya neema ya Mungu kuvuka mipaka ya kanisa. Janga la Covid-19 limekuwa mfano mmoja wa hivi karibuni wa jambo hili, na changamoto kubwa ya mabadiliko ya hali ya hewa ni mfano mwingine.

3.5 Katika ulimwengu wa vurugu kati ya dini na dini, jinsi tulivyo mawakala wa kufanya amani na majirani kutoka katika mani zingine ni kiini cha habari njema ya injili. Wito wetu wa kuwa mawakala wa kufanya amani unamaanisha pia kwamba tunapaswa kuamua kukataa na kupinga yote yaliyo ndani ya kanisa ambayo yanaweza kukuza kiburi na chuki kwa wale walio na tamaduni zingine za kidini

3.6 Katika ulimwengu unaoongezeka vizuizi vya uhuru wa kidini au imani, na kuongezeka kwa mateso ya Wakristo, jinsi Ushirika wa Anglican (kwa maneno ya Upendo wa Ukarimu) unaweza "kutoa mshikamano wetu na msaada kwa Wakristo ambao wanapaswa kushuhudia imani yao katika hali ngumu"[iii] huheshimu ufahamu wetu wa kuwa sehemu ya Mwili mmoja wa Kristo, katika huzuni na mateso, pia katika furaha na ufufuo.

3.7 Katika ulimwengu unaoongezeka vikwazo juu ya uhuru wa dini au imani, kuna ongezeko la fursa kwa Wakristo kufanya kazi na watu wa tamaduni nyingine za dini katika lengo la pamoja la kutetea uhuru huu, ikiwa ni pamoja na uhuru wa kubadili dini au imani ya mtu, na katika utetezi wa pamoja

**4 Maombi Maalum (Miito)**

Kulingana na dhamira yetu ya kufanya kazi kwa manufaa ya wote na wale wenye tamaduni na imani nyingine za kidini, kufanya amani katika jumuiya za kidini za ujirani, na mshikamano na dada na ndugu zetu katika Kikristo katika mazingira ya mapambano kwa ajili ya uhusiano baina ya imani, kwa hiyo tunatoa wito ufuatao:

4.1 Kwa sisi sote ambao ni wanafunzi wa Kristo, kushuhudia majirani zetu wa tamaduni zingine za kidini, kwa maneno na matendo, na kupitia huduma ya unyenyekevu.

4.2 Kwa Maaskofu katika Ushirika wa Anglikana, inapowezekana katika muktadha wa eneo lako, kujenga urafiki mpya na kiongozi wa desturi nyingine ya kidini, kuonyesha kujizatiti kwetu kufanya amani na manufaa ya wote

4.3 Kwa viongozi wa jumuiya nyingine za imani, kujiunga pamoja nasi katika kuchunguza jinsi tunavyoweza kuwezesha kazi ya ushirikiano zaidi katika kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na changamoto nyingine katika mazingira yetu ya pamoja, kupunguza umaskini na kuwajali walio katika mazingira magumu

4.4 Kwa Tume ya Uhusiano baina ya Imani ya Anglikana: kupata fedha kwa ajili ya utafiti wa makasisi au watendaji walei kutoka katika Ushirika wote wa Anglikana ndani ya utaratibu maalumu wa mahusiano baina ya imani kwa lengo la kukipatia rasilimali kizazi kipya cha wanazuoni watendaji wa Anglikana ili manufaa ya kujifunza teolojia kuhusu tamaduni nyingine za kidini yaweze kuthibitishwa na kukuzwa katika utume wa Ushirika mpana

4.5 Kwa maaskofu na majimbo ya Ushirika wa Anglikana, ambapo ni salama na inawezekana kuweka uhusiano na sehemu zile za Ushirika wetu zinazokabiliwa na uadui na mateso ili kuwe na ubadilishanaji wa habari, msaada wa maombi, na mshikamano katika urafiki, pamoja na msaada wa wale wanaokumbana na shida katika uamuzi wa kubadili dini yao na kuwa Wakristo.

4.6 Kwa sisi sote ambao ni wanafunzi wa Kristo, kujitolea kuliombea Kanisa linaloteswa katika juhudi zake za kuendelea kuhusika kwa upole na kushuhudia imani hata katikati ya uadui na mapambano ili kujenga uhusiano imara na majirani wa imani zingine

**5 Utekelezaji**

Tume ya Uhusiano baina ya Imani itakuza na kuhimiza:

- Njia za dhahiri za kufuatilia matokeo ya wito wa urafiki mpya katika dini (4.2)
- Njia za dhahiri za kufuatilia matokeo ya wito kwa hatua ya ushirikiano kwa wale wenye mila nyingine za kidini (4.3)
- Kuanzisha ufadhili wa utafiti: kamati iliyopewa jukumu la kusimamia hili, kushughulikia bajeti za programu za uzamivu, malazi, nk na kurudisha ujifunzaji na utekelezaji katika ngazi ya mahali husika, Jimbo na Ushirika (4.4)
- Utekelezekaji wa mipango ya kuoanisha: jinsi ya kutambua mazingira ya kutafuta mshikamano, jinsi ya kufanya hii isiwe rasmi: ni lazima ijengwe katika uhusiano uliopo wa kidayosisi au kutenganishwa au kuingiliana? (4.5)

## Melezo ya Mwisho

i. *Upendo wa Ukarimu: ukweli wa injili na wito wa mazungumzo, teolojia ya Anglikana ya mahusiano baina ya imani,* Lambeth Conference, ukurasa wa 10, inapatikana kwenye **https://www.acommonword.com/wp-content/uploads/2018/05/Generous_Love.pdf**

ii. *Upendo wa Ukarimu: ukweli wa injili na wito wa mazungumzo, teolojia ya Anglikana ya mahusiano baina ya imani,* Lambeth Conference, ukurasa wa 8, inapatikana kwenye **https://www.acommonword.com/wp-content/uploads/2018/05/Generous_Love.pdf**

iii. *Upendo wa Ukarimu: ukweli wa injili na wito wa mazungumzo, teolojia ya Anglikana ya mahusiano baina ya imani,* Lambeth Conference, ukurasa wa 10, inapatikana kwenye **https://www.acommonword.com/wp-content/uploads/2018/05/Generous_Love.pdf**

# WITO WA LAMBETH
# **MARIDHIANO**

*Mmwendee yeye, jiwe lililo hai, lililokataliwa na wanadamu, bali kwa Mungu ni teule, lenye heshima. 5Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za kiroho, zinazokubaliwa na Mungu, kwa njia ya Yesu Kristo... Bali ninyi ni uzao teule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu. Ninyi mliokuwa kwanza si taifa, bali sasa ni taifa la Mungu; mliokuwa hamkupata rehema, bali sasa mmepata rehema.*
*1 Petro sura ya 2, aya 4-10*

## 1 Utangulizi

Utume wa Mungu wa kupatanisha ni huduma ya Kanisa leo. Tuna shauku, na kujizatiti katika maridhiano kupitia rehema na neema ya Mungu inayookoa ndani ya Yesu, tukijua kabisa kwamba bila hiyo, sisi ni maskini. Tumekombolewa kama taifa takatifu na tumeitwa kufanya kazi na Mungu katika kuishi maridhiano haya.

## 2 Azimio

Tunamwamini Mungu ambaye ni mmoja katika utatu. Katika Utatu huu, umaalumu na umoja huwekwa katika moyo wa Mungu, kama Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Katika maisha, kifo, ufufuo, na kupaa kwa Yesu Kristo, Mungu humfikia binadamu aliyejitenga na aliyevunjika kwa kuwa mwili, akijiweka na kujipatanisha na binadamu kwa njia ya ajabu, ya kipekee. Katika upatanisho wa mwisho juu ya msalaba, Mungu katika Kristo anashuhudia gharama na maumivu yanayohusika katika kupatanisha. Kila mmoja ameumbwa kwa mfano wa Mungu kwa namna ya pekee na katika mazingira tofauti, tunaalikwa katika ushirikiano wa agano katika utume wa upatanisho wa Mungu. Tofauti zetu zilizojumuishwa katika Ushirika wa Anglikana zinatoa changamoto na kuimarisha uzoefu wetu juu ya Mungu kwa upande mwingine. Tunapojiunga na utume wa Mungu wa upatanisho kupitia Yesu kwa nguvu za Roho, utofauti wetu unafurahiwa na mgawanyiko wetu unakombolewa, kwa kuwa tumefanywa kamili katika mwili wa Kristo. Katika ukamilifu huo anuwai, tunaakisi kikamilifu sura ya Mungu.

## 3 Uthibitisho

3.1 Uhusiano katika utofauti unaweza kuwa mtakatifu na changamani. Tunatambua kwamba andiko, hasa andiko la msingi la 1 Petro la Lambeth Conference ya mwaka 2022, limetafsiriwa kwa muda mrefu na wale wanaotumia mamlaka, iwe katika mataifa, makanisa, tamaduni, au kaya, ili kusaidia utawala na ukandamizaji wa wanadamu wengine. Sisi ni washiriki katika mifumo inayoleta mgawanyiko, kutokubaliana, na migogoro kati yetu na ndani yetu. Maridhiano yanahitaji haki, uwajibikaji na mabadiliko katika jamii na katika Kanisa. Bila haya, ukandamizaji na mgawanyiko huendelea, ukipunguza ubinadamu wa wote walioshikwa katika mifumo hiyo, bila kujali wajibu wao. Tunamwomba Roho Mtakatifu atuwezeshe na kutuhamasisha tunapotafuta uhusiano sahihi katika Kristo, kati yetu, ndani ya kila mmoja wetu, na Mungu, pamoja na uumbaji.

3.2 Wito huu unathibitisha tena utume wa Mungu wa kupatanisha, mchakato unaoendelea wa kuturudisha kwa Mungu na kwa njia ya Kristo, kama huduma ya Kanisa. Kwa kutambua kwamba wale walio mamlakani wakati mwingine wametumia mazungumzo ya maridhiano ili kudumisha mifumo ya mamlaka na kuzuia juhudi za haki na ukamilifu, tunatafuta mtazamo wa Ushirika juu ya huduma hii kama ilivyo katika miktadha yetu tofauti.[i] Tunaposhuhudia pamoja, tunafanya mazoezi ya kupatanisha yaliyoangaziwa katika Lambeth Conference: kuwa wadadisi na kujiuliza kuhusu uzoefu wa kipekee wa kila mmoja; kuwepo kwa ajili ya kila mmoja, kusikiliza kwa makini na bila kuhukumu; na kutafakari upya miktadha yetu wenyewe kadiri uelewa wetu unavyopanuliwa kwa maombi.[ii] Tunatafuta kufanya mazoezi ya upatanisho katika kila nyanja ya maisha yetu, yanayoonekana na yasiyoonekana.

## 4 Maombi Maalum (Miito)

4.1 Tunatoa wito kwa Waanglikana ulimwenguni kote wamgeukie Mungu katika maombi kwa ajili ya kuburudishwa katika rehema na neema ya kipekee ya Kristo katikati ya mafarakano, mgawanyiko na utengano kati yetu na baina yetu. Tunahimiza ushirika na liturujia anuwai zinazotumiwa katika Ushirika wote wa Anglikana ambazo zinatualika kutubu na kufanywa upya na ambazo zinadhihirisha karama ya Mungu ya maridhiano.

4.2 Tunajizatiti kama maaskofu kuzitaka dayosisi zetu kujiunga katika desturi hii ya maridhiano katika Ushirika wote, kwa kutumia rasilimali zilizopo za maridhiano.[iii] Tunathibitisha 'Wito' kuhusu Mazingira na Malengo ya Maendeleo Endelevu na 'Wito' kuhusu Ekumeni kama mifano ya kujizatiti kwa Ushirika wote katika maridhiano kuhusiana na uumbaji wa Mungu na madhehebu mengine.

4.3 Tunajizatiti sisi wenyewe kama maaskofu kuhamasisha kizazi kijacho kwa kufurahia mchango wao katika huduma ya maridhiano na kukuza matumaini yao. Tutaweka mazingira ya kusikiliza na kujibu maumivu yao na maumivu ya kizazi, na kuwezesha ushiriki wao kamili katika mipango ya maridhiano.

4.4 Tunaalika seminari za Kianglikana na programu za mafunzo katika Ushirika, zikisaidiwa na Tume mpya ya Elimu ya Teolojia na Vyuo na Vyuo Vikuu vya mtandao wa Ushirika wa Anglikana, kuweka fursa za mafunzo na mazungumzo kuhusu maridhiano kama sehemu ya msingi ya utambulisho wetu kama wafuasi wa Kristo, kusikia haswa kutoka kwa wanateolojia katika maeneo ya Ushirika ambayo kihistoria yamekuwa na nguvu kidogo.

4.5 Tukitambua maumivu ya ubaguzi wa rangi, kiutamaduni na kitabaka, na kwa kuhamasishwa na kazi nyingi za makanisa ya Anglikana katika kusema ukweli na kukiubaliana na uhalisia, tunaalika kila Jimbo lifanye zoezi la kujichunguza na kutafakari, kusikiliza kwa heshima uzoefu wa wale ambao kihistoria wamekuwa na wa naendelea kutengwa katika mazingira yao na katika kanisa lao.[iv] Na tunatoa wito kwa kila Chombo cha umoja katika Ushirika wa Anglikana kufanya zoezi kama hilo la kujichunguza, la kusikiliza.

4.6 Tunapotambua umuhimu wa haki na uwajibikaji katika maridhiano ya Mungu, tunatoa wito kwa ACC kutoa muhtasari wa mpango wa kuelewa vizuri na kuhoji urithi wa ukoloni ndani ya Ushirika wa Anglikana. Hii inaweza kujumuisha, lakini si tu, desturi za kiutume zilizojengwa katika madhanio ya kibeberu, na mifumo ambayo inaendelea kuenzi ukoloni. Ni matumaini yetu itajengwa kwenye kazi ambayo tayari inafanywa kupitia ACC.

4.7 Tunamwomba Askofu Mkuu wa Canterbury, pamoja na Kamati ya Kudumu ya ACC [v], kufanya upya na kuhuisha mazungumzo na dada na kaka zetu katika majimbo na dayosisi zisizoweza kujiunga nasi katika Lambeth Conference 2022, wakitafuta kujenga maisha kamili pamoja kama familia ya makanisa ya Anglikana.

4.8 Tunatoa wito kwa Askofu Mkuu wa Canterbury, Maaskofu Wakuu, na ACC kuongeza wasifu wa njia na mitandao iliyopo ya ufadhili ambao utasaidia ujenzi wa amani na wale wanaosimama kwa ajili ya haki na ukamilifu katika majimbo yanayopitia mgogoro mkali.

## 5 Utekelezaji

5.1 Tunaomba kwamba kila jimbo lijihusishe na rasilimali ya upatanisho waliyoichagua kufikia Mkutano wa Maaskofu Wakuu wa mwaka 2025, ili kusimuliana simulizi kutokana na uzoefu huo na kutokana na kusikiliza makundi ambayo kihistoria yametengwa.[vi]

5.2 Tunaialika Tume ya Elimu ya Kiteolojia kusaidia seminari kuandaa fursa kwa ajili ya mazungumzo na kutoa ripoti ya matokeo yake katika ACC-19.

5.3 Tunaomba Vyombo vya Ushirika vipokee maswali na ushuhuda kutoka kila jimbo ili kuanza mazoezi yao ya kujichunguza. Tunatarajia watajibu kuzingatia hatua zilizopendekezwa ifikapo mwaka 2025.

5.4 Tunatarajia ACC kutoa ripoti katika ACC-19 kuhusu maendeleo yake na, na mipango kwa ajili ya kujifunza urithi wa kihistoria wa ukoloni kwa macho safi na kuhoji matendo ya kiutume ambayo bado yanaweza kuwa msingi katika mawazo na desturi za kibeberu, na mifumo ambayo inaweza kuendelea kuenzi ukoloni, kufanya kazi na Mtandao wa Wazawa Waanglikana na wengine wanaoishi wakiwa na athari zinazoendelea za ukoloni.

5.5 Tunakaribisha kazi ya ujenzi wa amani ya timu ya Maridhiano ya Askofu Mkuu wa Canterbury, ikifanya kazi na Mfuko wa Ushirika wa Anglikana na Mtandao wa Amani na Haki wa Anglikana, kuripoti kwa maaskofu wakuu juu ya njia za kuonesha mwitikio wa ujenzi wa amani na usaidizi kwa wajenzi binafsi wa amani kwenye majimbo yanayokabiliwa na mzozo mkali.

5.6 Tunamwomba Askofu Mkuu wa Canterbury na Kamati ya Kudumu ya ACC [vii] kuripoti kuhusu mazungumzo mapya na majimbo na dayosisi ambazo hazikuweza kujiunga nasi Lambeth 2022 katika ACC-19.

5.7 Tunaomba kwamba Mtandao wa Vijana wa Ushirika wa Anglikana na timu ya Maridhiano ya Askofu Mkuu wa Canterbury watoe mawazo ya kuwashirikisha vijana katika mipango ya upatanisho mara tu inapofaa na kufurahia kile ambacho kimeendelezwa na vijana katika ACC inayofuata.

## Melezo ya Mwisho

i. Tunakubali kwamba neno 'maridhiano' limejaa katika muktadha fulani, aidha kuashiria eneo moja la uhusiano uliovunjika na/au kuwa la kisiasa lisilosaidia. Pia tunagundua kuwa dhana ya maridhiano inaonyeshwa tofauti kati ya muktadha tofauti. Kwa mfano, neno *maridhiano* linaweza kuwa na maana ya upatanisho ikimaanisha kwamba pande mbili zinakutana na kusonga mbele pamoja. Huko Fiji, maridhiano huonyeshwa kwa kutoa msamaha kama zawadi. Ikiwa itapokelewa kwa unyenyekevu, kuna maridhiano na kukumbatiwa. Nchini Kongo, dhana hii inaonyeshwa kupitia neno linalomaanisha *urithi wa pamoja*.

ii. Kwa taarifa zaidi kuhusu mazoea haya, angalia makala ya *Ministry* in a contlicted-world/the-course/ kwa ajili ya maandalizi ya Lambeth Conference: **https://www.lambethconference.org/programme/ministry-in-a-conflicted-world/the-course/**

iii. Nyenzo zinaweza kujumuisha zile zinazopendekezwa na Majimbo ya Anglikana au Mitandao ya Anglikana k.m Mitandao ya Anglikana ya Wazawa, au Mtandao wa Amani na Haki wa Anglikana au kozi ya Difference kutoka katika Huduma ya Maridhiano ya Askofu Mkuu wa Canterbury na kitabu chake kiitwacho *'The Power of Reconciliation'*.

iv. Kwa mfano, Kanisa la Anglikana la Kanada, Kanisa la Anglikana la Aotearoa, New Zealand na Polynesia, na kazi ya hivi karibuni iliyofanywa kuhusu ubaguzi wa rangi na kasumba ya watu weupe katika Kanisa la Kiaskofu.

v. Kamati ya Kudumu inawajibika kwa kazi inayoendelea ya ACC katika mikutano ya mwili wote.

vi. Nyenzo zinaweza kujumuisha zile zinazopendekezwa na Majimbo ya Anglikana au Mitandao ya Anglikana k.m Mitandao ya Anglikana ya Wazawa, au Mtandao wa Amani na Haki wa Anglikana au kozi ya *Difference* kutoka katika Huduma ya Maridhiano ya Askofu Mkuu wa Canterbury na kitabu chake kiitwacho *'The Power of Reconciliation'*.

vii. Kamati ya Kudumu inawajibika kwa kazi inayoendelea ya ACC katika mikutano ya mwili wote.



LAMBETH CONFERENCE

www.lambethconference.org
info@lambethconference.org

**Fuatilia mazungumzo**
www.facebook.com/LambethConference
www.twitter.com/LambethConf
#LambethConf

Kilichapishwa Mei 2023, kama sehemu ya awamu ya tatu ya safari ya Lambeth Conference